**Tanzania** kinara wa uwekezaji nchi za EAC kwa dola bil. 1

UKURASA 2



**Vituo** 26 vya mafuta vyafungiwa kwa madai ya uchakachuaji

UKURASA 3


Umemejua unavyokoleza uwekezaji vijijini, shuleni

Siasa za Bongo ziwe sawa na Simba, Yanga

BUFE

Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

KUOZA MATUNDA, MBOGA
Wakulima, wafanyabiashara wataka viwanda na miundombinu kuhifadhi

CPB inapowatangazia neema walima mahindi

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Agosti 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580671

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Aliyefungua kesi tozo za miamala aitwa Uhamiaji


Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la CILAO, Odero Odero

UKURASA 2



## SABAYA ANA KESI YA KUJIBU

- **KUJITETEA** binafsi, shahidi mmoja na vielelezo kadhaa...

*Endelea ukurasa 2*

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akishuka kwenye gari la Magereza, kwenda kusikiliza kesi ya jinai inayomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.
**PICHA: ALLAN ISACK**

UKURASA WA 3

## WATANZANIA 140,000 WAPATA CHANJO DHIDI YA CORONA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema hadi Agosti 10, mwaka huu, Watanzania 140,000 walikuwa wamepatiwa chanjo ya ugonjwa wa corona kwa awamu ya kwanza.
Alitoa takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mdahalo wa kitaifa kuhusu corona, uliohusisha taasisi za serikali, wataalamu wa afya na waandishi...



UKURASA WA 4

## SIMBACHAWENE ATAKA MAOMBI KUKABILI USHOGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewaomba viongozi wa dini kuongeza maombi ili kukomesha vitendo vya ushoga vinavyozidi kuongezeka nchini.
Alitoa rai hiyo jana wakati akifungua kongamano la wanawake waombolezao kitaifa kwa ajili ya...

UKURASA WA 5

## MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA YATUMIA BAJETI KUBWA

SERIKALI imesema kuwa sehemu kubwa ya bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hutumika kukabili magonjwa yasiyoambukiza, hata hivyo, kiwango hicho hakitoshi kuleta matokeo chanya...

# Mashahidi na vielelezo dhidi ya Mbowe kujulikana leo

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YACHEZA KARATA 2021/22 UK. 24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Aliyefungua kesi ya kupinga tozo miamala aitwa Uhamiaji

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MWANAHARAKATI Odero Charles amesema amepokea wito wa Idara ya Uhamiaji unaomtaka kwenda kujieleza kuhusu uraia wake.

Odero ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Uraia na Msaada wa Kisheria la CILAO, aliithibitishia Nipashe jana kuhusu taarifa za kuitwa kwake na idara hiyo.

Mwanaharakati huyo alisema kuwa alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kwake kuwa ni Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Arusha na kumtaka afike ofisini kwake.

"Ni kweli nilipigiwa simu Agosti 11 mwaka huu nikatakiwa kufika Ofisi za Uhamiaji Mkoa wa Arusha, ninahitajika kujibu kuhusu uraia wangu. Wala siogopi na nitatii wito huo wa kwenda kwenye ofisi hizo kama walivyonihitaji," alisema Odero

Hata hivyo, wakati akizungumza na Nipashe jana, Odero alidai, alikuwa Dar es Salaam ambako wiki iliyopita alifungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kupinga tozo za miamala ya simu.

Kuhusu taarifa zinazozagaa katika mitandao ya kijamii kwamba anashikiliwa na Ofisi za Uhamiaji na kunyang'anywa simu zake, Odero alizikanusha kwamba hazina ukweli.

Kesi ya kupinga tozo za miamala ya simu aliyofungua mwanaharakati huyo imepangwa kusikilizwa na Jaji John Mgeta leo.

**OFISA UHAMIAJI**

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Arusha, Hoseah Kagimbo, alikiri kumpigia simu Odero kumwita ofisini kwake.

Hata hivyo, ofisa huyo alisema kuwa licha ya kumwita, Odero hajaripoti ofisini huko kwa madai kuwa kwa sasa yuko jijini Dar es Salaam.

Alibainisha kuwa baada ya kupewa majibu hayo na Odero kwamba yuko Dar es Salaam, alimtaka mwanaharakati huyo aripoti Ofisi za Uhamiaji ziliko huko aliko.

"Mimi nilimpigia simu kumwita hapa, lakini habari za kusema tumemtaka aje na kitambulisho cha NIDA (Kitambulisho cha Taifa), hati za kusafiria na cheti cha kuzaliwa, siyo kweli.

"Sijatoa maelekezo hayo zaidi ya kumtaka aje hapa na alipodai yuko Dar es Salaam, nikamwelekeza aende Ofisi za Uhamiaji huko aliko, hayo mengine sijui yanatoka wapi," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu taarifa ya uwekezaji nchini katika kipindi cha mwaka 2020/2021. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sabaya akutwa na kesi ya kujibu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imewakuta na kesi kujibu aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na washtakiwa wenzake wawili.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo la jinai namba 105 ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura, wanaokabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Hakimu Mwandamizi wa mahakama hiyo, Odira Amworo, alisema washtakiwa wote watatu wana kesi ya kujibu katika mahakama hiyo.

Hakimu alisema kuwa baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na kuwasilishwa mahakamani huko, washtakiwa wote wana kesi ya kujibu, hivyo kila mmoja anatakiwa kujitetea.

"Washtakiwa baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na kuwasilishwa mahakamani mna kesi ya kujibu na kuna njia mbili za kujitetea ambazo ni chini ya kiapo au kuwa na mashahidi," alisema.

Wakili wa Mshtakiwa wa Kwanza, Dancan Oola, alidai mahakamani huko kwamba Ole Sabaya atajitetea mwenyewe chini ya kiapo na tangu alipozungumza naye mara ya mwisho, alimweleza kwamba ana shahidi mmoja.

Hata hivyo, wakili huyo alidai mahakamani huko kwamba watakuwa na mashahidi wasiozidi wawili.

Wakili wa mshtakiwa wa pili, Edmund Ngemela, alidai mahakamani huko kwamba mteja wake, Nyegu, atajitetea kwa njia ya kiapo na atakuwa na shahidi mmoja.

Fridolin Gwemelo, Wakili wa mshtakiwa wa tatu, Mbura, alidai mteja wake atajitetea chini ya kiapo na atakuwa na baadhi ya vielelezo ambavyo atawasilisha mahakamani huko.

Awali akiwasomea mashtaka washtakiwa hao, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, alidai shtaka la kwanza ni la unyanganyi wa kutumia silaha linalowakabili washtakiwa hao.

Wakili Chavula alidai washtakiwa hao Februari 9 mwaka huu, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. milioni 2.769, mali ya Mohamed Saad na baada ya wizi huo, walitumia silaha ya bunduki kuwatisha waliokuwa kwenye duka hilo.

Shtaka la pili ni la unyanganyi wa kutumia silaha, ikidaiwa mahakamani huko kwamba washtakiwa hao kwa pamoja, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi na baada ya wizi huo walimfunga kwa pingu, kumpiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kwake.

Shtaka la tatu ni la wizi wa kutumia silaha, ikidaiwa mahakamani huko kwamba Ole Sabaya na washtakiwa wenzake hao, Februari 9 mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja aina Tekno Pop na fedha kiasi cha Sh. 35,000, mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wapatiwe fedha na mali walizoiba.

Katika kuijenga kesi hiyo, Upande wa Jamhuri ulipeleka mahakamani mashahidi 11 na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za ushahidi ikiwamo picha za mnato na barua za ushahidi zinazoonyesha mchakato wa upelelezi wa shauri hilo ulivyofanyika.

Hakimu Amworo aliahirisha shauri hilo hadi leo, washtakiwa hao watakapoanza kujitetea mahakamani huko.

## Tanzania kinara uwekezaji EAC kwa dola bil. 1

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA imezipiku nchi zote za Afrika Mashariki kwa kupata uwekezaji mkubwa wa Dola bilioni 1.0, kwa mujibu wa taarifa ya uwekezaji ya kidunia iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Biashara Sawia Kimataifa (UNCTAD).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya uwekezaji wa kidunia kwa mwaka 2020, Burundi ilipata uwekezaji wa Dola million sita, Kenya Dola milioni 717, Rwanda Dola milioni 135 na Uganda Dola milioni 823.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, alisema jana kwamba janga la corona imesababisha Tanzania kuvutia mitaji ya viwanda vya dawa za binadamu hususani vifaa vya kujikinga (PPE).

Kuhusu ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji, Dk. Kazi alisema katika kipindi cha mwaka wa 2020/21 miradi ya wawekezaji ya Watanzania pekee iliyosajiliwa ni 66 sawa na asilimia 28 ya miradi yote 235 kwa kipindi hicho.

Pia alisema miradi ya ubia kati ya Watanzania na wageni iliyosajiliwa ni 65 sawa na asilimia 28 ya miradi yote, hivyo katika miradi 235 iliyosajiliwa, asilimia 56 ya miradi hiyo Watanzania wamehusika katika umiliki wake.

Alisema kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika kipindi cha mwaka 2020/21 kumekuwapo mafanikio makubwa katika eneo la uwekezaji ambayo ni kusajiliwa kwa miradi mipya 235 inayotarajia kuwekeza mtaji wa Dola za Marekani bilioni 3.3 na kuzalisha ajira mpya 36,849.

Idadi hiyo, alisema ni ongezeko la asilimia nane ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2019/20 ambapo ilisajiliwa miradi 219 na kwamba miradi miradi 99 iko Dar es Salaam ikifuatiwa na Pwani 34.

Mikoa mingine na idadi ya miradi kwenye mabano ni Mwanza (15), Dodoma (13), Arusha (120, Shinyanga (11), Mara (tisa), Iringa na Tanga (minane) kila mmoja, Morogoro (saba), Geita (minne), Lindi na Ruvuma (mitatu kila mmoja), Kagera (miwili) na mikoa iliyobakia mradi mmoja kila mmoja.

Dk. Kazi alisema sekta ya uzalishaji viwandani yenye miradi 138 ikiongoza kwa uwekezaji.

Alisema kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kumechangiwa na jitihada zilizofanywa na uongozi wa serikali ya awamu ya sita akitoa mfano wa Aprili hadi Juni, mwaka huu ambapoTIC ilisajili miradi 84 ambayo ni ongezeko la asilimia 68 ikilinganishwa na miradi 50 kipindi kama hicho mwaka jana.

Pia alisema ajira na mitaji inayotarajiwa kutokana na miradi ya Aprili hadi Juni ni wastani wa mara sita ikilinganishwa na kipindi hicho mwaka jana na kwamba kuongezeka kwa miradi, ajira na mitaji hiyo inatokana na maboresho mbalimbali yaliyofanywa na TIC.

HABARI KITAIFA

## Watanzania 140,000 wapata chanjo dhidi ya corona

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema hadi Agosti 10, mwaka huu, Watanzania 140,000 walikuwa wamepatiwa chanjo ya ugonjwa wa corona kwa awamu ya kwanza.

Alitoa takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mdahalo wa kitaifa kuhusu corona, uliohusisha taasisi za serikali, wataalamu wa afya na waandishi wa habari.

Dk. Gwajima alisema baada ya kupokea chanjo ya Johnson & Johnson, serikali itapokea chanjo zingine nne kwa ajili ya matumizi ambazo ni Pfizer, Moderna, Sinopharms na Sinovac.

Alisema awamu ya pili ya chanjo ya mpango maalumu kwa nchi maskini COVAX, itawasili nchini wakati wote ndani ya mwezi huu.

Hivyo, aliwataka wananchi waliopo maeneo mbalimbali nchini kujitokeza kupatiwa chanjo baada ya awamu ya kwanza ya dozi milioni moja ya Johnson & Johnson kuwalenga makundi maalum.

"Awamu ya kwanza iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan ililenga makundi maalum na kwamba COVAX itawafikia Watanzania milioni 11 kama ilivyopangwa," alisema Dk. Gwajima.

"Wananchi waende kupata chanjo sababu ni neema kwetu kama dunia. Imepatikana muda mfupi tangu virusi hivi kuingia duniani ni fursa kwetu ili kupunguza vifo, dunia imeshuhudia zaidi ya vifo milioni nne hadi sasa.

"Ikumbukwe yalikuwapo magonjwa makubwa yaliyoikumba dunia tangu hatujazaliwa, zamani kama vile polio, surua, ndui yakatolewa chanjo. Je, waliokuwapo wasingetuchanja pengine wengine tusingekuwa hapa?" Alihoji.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Balozi wa Oman hapa nchini aliyemaliza muda wake, Ali Bin Abdallah Bin Salim Al Mahrouqi, aliyefika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana kwa ajili ya kuaga. **PICHA: IKULU**

# Mashahidi, vielelezo kesi ya Mbowe kujulikana leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu leo inatarajia kusikiliza maelezo ya ushahidi, idadi ya mashahidi na vielelezo katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Kesi hiyo imepangwa kuja mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwa ajili ya upande wa mashtaka kuwasomea washtakiwa maelezo ya ushahidi.

Upande wa Jamhuri pamoja na kusoma ushahidi huo, pia utataja na kuorodhesha idadi ya mashahidi wanaotarajia kutoa ushahidi wao na idadi ya vielelezo watakavyowasilisha na baadaye kesi kuhamishiwa Mahakama Kuu kwa kuanza kusikilizwa.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Mahakama kufahamishwa kwamba upelelezi umekamilika, jalada liko kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya maelekezo, ili kuandaa taarifa, kwa ajili ya kesi hiyo kuhamia Mahakama Kuu.

Agosti 6, mwaka huu, Jamhuri iliwasomea washtakiwa mashtaka mapya sita na Mahakama iliamuru waletwe baada ya siku saba kwa ajili ya kusomewa maelezo ya mashahidi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, Christopher Msigwa na Sylvia Mitanto.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na Peter Kibatala, Lwekamwa Rweikiza, John Mallya, Fredrick Kihwelo, Selemani Makoweka, Michael Rugina, Iddi Msawanga, Jebra Kambole na Sisty Aloyce.

Wakili Hillar, alidai Julai 26, mwaka huu Mbowe alisomewa mashtaka akiwa peke yake na Julai 27, washtakiwa wengine watatu waliokuwa katika kesi hiyo waliachiwa na kufanya idadi ya washtakiwa kubakia wanne badala ya saba.

Wakili Hillar aliwasomea mashtaka sita ya ugaidi tofauti na hati ya mashtaka ya awali iliyofunguliwa Agosti mwaka 2020, ikiwa na mashtaka 13.

Hillary aliwataja washtakiwa kuwa ni Mbowe, Halfan Hassan, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Lingwenya, ambao wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 63/2020.

Alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita, katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katila Hoteli ya Aishi, iliyopo Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Lingwenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika shtaka la tatu mshtakiwa Halfani, Adamu na Lingwenya, wanashtakiwa kwa kukusanya fedha kutoka kwa Mbowe wakiamini zitasaidia kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko.

Shtaka la nne, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger, bila kuwa na kibali. Katika shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa siku na mahali hapo alikutwa na vilipuzi ambavyo ni risasi tatu, bila ya kuwa na leseni.

Mshtakiwa Halfani anadaiwa Agosti 10, 2020, kwa nia ya kuhatarisha usalama wa nchi alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana, koti la mvua, jacket, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

# Vituo 26 mafuta vyafungwa kwa madai ya uchakachuaji

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji (EWURA) imevifungia vituo 26 vya kuuza mafuta baada ya kubainika kufanya njama za kuuza mafuta yasiyo na vinasaba vinavyokidhi vigezo.

Vilevile, vituo hivyo vimebainika kufanya udanganyifu wa kukwepa kodi kwa kuchanganya mafuta yaliyolipiwa kodi na yasiyolipiwa kodi.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Godfrey Chibulunje, alisema mbali na kuvifungia, pia imevitoza faini.

Chibulunje alisema vituo hivyo vilivyofungiwa ni vya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati ambavyo vilibainika baada ya mamlaka hiyo kufanya ukaguzi Julai mwaka huu.

"Hii inamaanisha kuwa wamiliki wa vituo hivyo walichanganya mafuta yao na ambayo hayajalipiwa kodi stahiki ya serikali.

"EWURA imechukua hatua stahiki kwa wafanyabiashara hao ikiwa ni pamoja na kufunga vituo vyote vilivyokutwa na mafuta yasiyo na vinasaba na kulipishwa faini kwa mujibu wa kanuni," alisema Chibulunje.

Alisema mamlaka hiyo ilianzisha mradi wa uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta yanayotumika katika soko la ndani mwaka 2010 kwa lengo la kutofautisha mafuta yaliyolipiwa kodi na yale yasiyolipiwa.

"Kwa mujibu wa kanuni, kampuni zenye depots zinatakiwa kuhakikisha mafuta yote yanayonunuliwa kwa ajili ya soko la ndani yanawekwa vinasaba," alisema Chibulunje.

Alivitaja vituo vilivyofungiwa kuwa ni pamoja na Total Tanzania Ltd (Ukuni, Bagamoyo), Asam Oil Company Ltd (Kisemvule), South Mark Oil (Mkuranga).

Vingine Kitange Oil Company LTD (Dodoma), Camel Oil Ltd (Chamazi, Temeke), Olympic Petroleum Ltd (Tunduma), Petroafrica Tanzania (Momba), Gapco Ltd (Tunduma) na Camel Oil Ltd (Tunduma).

Shiuya Co Ltd (Mbozi), Mnyonge Investement Co.Ltd (Momba), Mabena Filling Station (Momba), Admire Oil Ltd (Mbeya), Furahisha Franci Msigwa (Makambako) na Ahmed Basaleh Petrol Station (Njombe).

Vingine ni Oilcom Mwanza Filling Station (Nyamagana), Total Ltd (Nyamagana), GBP Tanzania (Nyamagana).

Front Oil Service Station (Kahama), Oryx Oil Co.Ltd (Bukoba), EAFCO (Bukoba), Remigius Patrick Nshange Petrol Station (Bukoba).

Vilevile, Lake Oil Ltd (Geita), GBP Ltd (Sengerema) na Lake Oil Ltd (Shinyanga).


## SHUKRANI

116405002

**Norah Michael Ngirwamungu**
**(kuzaliwa 30 mei 1967; kutwaliwa 14 julai 2021)**

Familia ya marehemu Dr Michael na Philomena Ngirwamungu inatoa shukrani za dhati kwa ndugu jamaa na marafiki pamoja na uongozi na jumuiya ya Dar Es Salaam University College of Education(DUCE) kwa faraja na missada mbalimbali wakati wote wa kuomboleza na mazishi ya mpendwa wetu Norah Michael Ngirwamungu.

Marehemu Norah alifariki siku ya jumatano,14 julai na kupumzishwa kwenye nyumba yake ya milele siku ya jumamosi,17 julai 2021.

Familia inatoa **shukrani maalumu kwa paroko,father Mario Dias wa kanisa katoliki la Mt. Immaculata,** upanga, Dar Es Salaam akisaidiana na father Menrard kalikawe kwa kuongoza ibada.

Tunawashukuru sana wana kwaya wa kanisa la Mt.Immaculata kwa nyimbo za faraja.

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa MS Clara Kanza,Dr Redemptor Mbatia na marafiki wa karibu wa marehemu Norah ikiwa ni pamoja na Zanaki Group na JKT Miaka 25 Group.

Kwa kuwa ni vigumu kumtaja akila mmoja alieungana nasi wakati wa msiba, familia inaomba nyote mpokee shukrani hizi za dhati kwa faraja kubwa mliyotupa.

BWANA AMETOA NA BWANA AMETWAA, JINA LAKE LIHIMIDIWE




Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa iliyofanyika jijini Dodoma jana kwa kuwashirikisha vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Magonjwa yasiyoambukiza yatumia bajeti kubwa

**Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kuwa sehemu kubwa ya bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hutumika kukabili magonjwa yasiyoambukiza, hata hivyo, kiwango hicho hakitoshi kuleta matokeo chanya kutokana na ukubwa wa tatizo hilo nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima amebainisha hayo jana, wakati akifungua mkutano wa kwanza wa meza ya majadiliano kuhusu namna ya kutafuta fedha, ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza (NCD) nchini.

Alisema kuwapo kwa ugonjwa wa Covid-19, kumeongeza mzigo huo kwa serikali kuwa mkubwa zaidi na kwamba ipo haja ya kukaa chini kutafuta ufumbuzi wa haraka.

"Kuongezeka kwa magonjwa mengine kama Covid-19 kunachangia NCD kuongezeka na hali kuwa mbaya zaidi nchini. Magonjwa hayo yanachukua sehemu kubwa ya bajeti kwani serikali inakuwa na mizigo miwili hivyo kushindwa kuimudu," alisema Dk. Gwajima.

Alisema hali hiyo ndiyo imewasukuma wataalam wa afya pamoja na wadau wa afya nchini kukutana kwa majadiliano, ili kuja na mbinu zitakazoisaidia serikali kupitia watunga sera kubuni njia rahisi zitakazotumia fedha kidogo kukabiliana na tatizo hilo.

"Sasa tunawaambia wataalam wetu wajadili namna ya kutumia fedha kidogo kuyakabili magonjwa hayo," alisema Dk. Gwajima huku akiwataka kubuni mbinu zitakazosaidia kupata vyanzo vya fedha, ili kuiwezesha serikali kupunguza kuwategemea wafadhili kutoka nje wakati wote.

Alisema serikali itaendelea kukabili matatizo ya afya kwa wananchi wake nikiwamo NCD na kwamba sera ya serikali inalenga kuongeza uwezo wa kukabili magonjwa hayo, ingawa vyanzo vilivyopo havitoshi.

Kwa mujibu wa waziri huyo wa afya, takwimu za hivi karibuni zinaonyesha asilimia 33 ya Watanzania wanaugua magonjwa yasiyoambukiza na kwamba takwimu hizi zinatisha na kuhitaji umakini zaidi katika kuyakabili.

Alifafanua kuwa asilimia 16 ya Watanzania wenye umri kati ya miaka 30 hadi 70 wanakufa kutokana na NCD na aliwataka wataalam hao kutoka na maazimio yanayolenga kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Dk. Gwajima, pia aliwataka wataalam hao kuandika maazimio ya mkutano huo katika lugha rahisi ambayo itaeleweka na wananchi, ili waelewe namna bora ya kujiepusha wasiugue na pia kujua njia za kuyadhibiti.

Mkutano huo umehudhuriwa na wataalam wa afya, watafiti, watoa huduma wa afya, kampuni za bima, wadau wa maendeleo, taasisi za fedha na mashirika yasiyo ya kiserikali.

**"Sasa tunawaambia wataalam wetu wajadili namna ya kutumia fedha kidogo kuyakabili magonjwa hayo," alisema Dk. Gwajima huku akiwataka kubuni mbinu zitakazosaidia kupata vyanzo vya fedha, ili kuiwezesha serikali kupunguza kuwategemea wafadhili kutoka nje wakati wote.**

# Kesi ya kusafirisha binadamu yakwama

**Na Hadija Kitwana**

UPANDE wa Jamhuri umeshindwa kusoma hoja za awali katika kesi ya biashara haramu ya kusafirisha binadamu inayomkabili raia wa Misri, Mohamed Shalaby na mwenzake baada upande wa utetezi kuomba muda wa kukutana na mteja wao.

Kesi hiyo ilikuja jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Kisutu, Godfrey Isaya, kwa ajili ya washtakiwa waliobaki, Mohamed na Fikirina kusomewa hoja za awali.

Wakili wa mshtakiwa wa kwanza Mohamed Hussein Hamisi, aliomba mahakama apate muda wa kukutana na mteja wake waongee, ili ajue nini atamshauri.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, haukuwa na pingamizi katika ombi hilo la wakili Hussein.

Hakimu Isaya aliahirisha kesi hiyo hadi Agost 26, mwaka huu kwa ajili ya kusoma hoja za awali na washtakiwa walirudishwa rumande.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Fikirina Makubi ambaye anakabiliwa na shtaka la kujihusisha katika mpango wa biashara haramu ya kuuza binadamu ambapo hapo awali kulikuwa na washtakiwa watano ambao watatu walikiri makosa yao na kuhukumiwa kifungo au faini.

Ilidaiwa kuwa Agosti 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam washtakiwa walikamatwa kwa tuhuma za kufanya biashara haramu ya kuuza binadamu.

# Watu 500 kuajiriwa kiwanda cha chaki

**Na Happy Severine, MASWA**

WATU 500 wanatarajia kupata ajira katika kiwanda cha chaki cha Halmashauri ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu baada ya kuanza uzalishaji.

Kiwanda hicho ambacho ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, chini ya kampuni ya Ng'hami Industrial Company, kinatarajiwa kuongezea mapato ya halmashauri.

Halmashauri hiyo inatarajia kupata mapato yanayofikia zaidi ya Shilingi bilioni tano kwa mwaka kitakapoanza uzalishaji.

Hayo yalisemwa jana na aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Fredrick Sagamiko, wakati wa makabidhiano ya ofisi na mali kwa mkurugenzi mpya, Saimon Berege yaliyofanyika mjini Maswa.

Dk. Sagamiko alisema kiwanda hicho kitakapoanza uzalishaji, ajira 500 zitatolewa ndani na nje ya Mkoa wa Simiyu na mapato ya halmashauri hiyo yataongezeka na kufikia Shilingi bilioni tano kwa mwaka.

Kadhalika, alisema ndani ya kiwanda hicho kipo cha kutengeneza vifungashio vya aina mbalimbali.

Aidha, alimuomba Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Berege, kuendelea kusimamia uendeshaji wa miradi yote iliyopo ndani ya halmashauri.

Kwa upande wake, Berege alisema yuko tayari kuendeleza na kutekeleza miradi yote iliyoachwa na msimamizi wake.

Alisema anahitaji ushirikiano wa dhati kutoka kwa watumishi wa umma ili kwa pamoja waijenge halmashauri hiyo.

The Guardian Limited

VACANCY

Freelance Sales Executives

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

616387602

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa ya kurasimisha makazi ichangamkiwe

**MOJA** ya mambo ambayo serikali inakazania na kuyawekea msukumo, ni kuhimiza wananchi kurasimishaji mkazi yao, kwa kuwa hatua hiyo itawanufaisha wanapokuwa wanamiliki ardhi ambayo imepimwa.

Kwa kawaida, ardhi iwe kiwanja au nyumba thamani yake hupanda pale inapokuwa imepimwa na maana ya kupima ardhi ni kuirasimisha, hivyo faida nyingi hupatikana baada ya ardhi kurasimishwa.

Baadhi ya faida ambazo mtu anaweza kuzipata baada ya urasimishaji, ni ardhi hupanda thamani yake, kuwa na sifa ya kukopesheka katika benki na taasisi za fedha kwa urahisi. Ardhi kutumika kama dhamana mahakamani, lakini kubwa ni mmiliki kuwa na uhakika kuwa anaimiliki kihalali na kisheria.

Kadhalika, urasimishaji ni kazi shirikishi inayowezesha wananchi kukubaliana mipaka ya viwanja, kufungua njia na kutoa maeneo ya huduma za jamii kama shule, barabara vituo vidogo vya polisi, makaburi, zahanati na maeneo ya wazi.

Kutokana na umuhimu huo, Benki ya NMB imezindua huduma mpya ya mkopo wenye riba nafuu wa kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini kutekeleza takwa la kisheria la kurasimisha makazi yao.

Huduma hiyo iliypewa jina la 'NMB Plot Loan' inaendeshwa kwenye Programu ya Kitaifa ya Urasimishaji wa Makazi ikitekelezwa kwa ushirikiano kati ya benki hiyo na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Benki hiyo itawasaidia wananchi kulipia gharama zote za urasimishaji wa makazi kuanzia upimaji wa viwanja mpaka uandaaji wa hatimiliki, na kwamba mwananchi atalipa kidogo kidogo ndani ya miaka miwili.

Aidha, riba ya mkopo huo inatajwa kuwa ni asilimia 10, na kwamba mwananchi atapatiwa hatimiliki baada ya kukamilisha urejeshaji wa mkopo wake katika benki hiyo.

Sisi tunaona kuwa hiyo ni fursa nzuri kwa kuwa inawawezesha wananchi wa kipato cha chini kumiliki makazi ambayo yanatambulika kisheria, hivyo tunawashauri kuichangamkia, kwa ajili ya faida yao, kwa kuzingatia kuwa kwa sasa ardhi ni mali hasa inapokuwa imepimwa.

Mtu anaweza kutumia adhi yake kukopa fedha benki na kufanyia shughuli za maendeleo au akiamua kuuza kwa bei nzuri, hivyo tunaamini kuwa suala la kurasimisha ardhi lina umuhimu mkubwa na wa kipekee ambao kila mwananchi hanabudi kuuchangamkia.

Ni jambo lililo dhahiri kwamba Watanzania wengi wanaoshindwa kurasimisha makazi yao kwa kukosa fedha za kulipia gharama za urasmishaji, lakini tunaona kuwa kupitia uwezeshaji wa mkopo NMB, utawaondolea hali ya unyonge na kuwapa unafuu wenye nia ya kurasimisha makazi yao.

Tunaipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuendeleza ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia sekta ya ardhi, hatua yake ya kushirikiana na NMB itekeleza mpango huo inathibitisha umakini na weledi wa viongozi wakuu wa wizara hiyo.

Changamoto iliyobaki sasa ni ya utoaji wa elimu na uhamasishaji wa wananchi kuielewa programu hiyo kisha kuanza taratibu za kukopa fedha kwa ajili ya urasimishaji wa makazi yao.

Tunadhani kwamba mpango huo ni mzuri na unapaswa kuwa endelevu ili kila wakazi wananchi wawe wakirasimisha makazi yao kwa lengo la kunufaika kama tulivyoeleza awali. Kupitia mpango huu, maeneo mengi ya Tanzania yatarasimishwa tofauti na sasa ambapo maeneo mengi hayajarasimishwa na kutambuliwa kisheria.

Hata hivyo, jambo la msingi ambalo wahitaji wa mkopo huo watatakiwa kulizingatia ni kuelewa kwamba fedha watakazopewa sio zawadi, bali ni mkopo kutoka kwa walipakodi wa nchi hii, hivyo watawajibika kuzirejesha baada ya urasimishaji wa makazi yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Sabato Kasika

Muungwana Lazima Nilonge

# Halmashauri ziseme zinapokwamia kutenga maeneo ya wamachinga

**WAMACHINGA** ni miongoni mwa wafanyabiashara muhimu katika kukuza uchumi, na pia ni suluhisho la mahitaji kwa Watanzania wengi kuanzia wale wa kipato cha chini, kati na cha juu.

Sekta hiyo inaelezwa kuwa na watu takribani milioni 3.1, huku takwimu za viwanda na biashara kwa upande wa viwanda vidogo na biashara ndogo ikiwa imetengeneza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika taarifa yake ambayo amewahi kuitoa wakati akizungumza kwenye kikao cha viongozi wa wamachinga, jijini Dar es Salaam.

Kwamba, watu walioajiriwa katika sekta hiyo ni asilimia 23.4 ya nguvukazi ya taifa na imechangia asilimia 27 katika pato la taifa na kuelezea jinsi ambavyo serikali inatambua umuhimu wa wafanyabiashara hao wadogo.

Hata hivyo, wakati serikali ikitambua na kuthamini mchango wao katika kukuza pato la taifa, bado halmashauri hazijawawekea mazingira rafiki ya kufanyia biashara, hali inayosababisha wahangaike huku na kule kila mara.

Kwa kumbukumbu zangu ni kwamba, serikali ilishawahi kuzielekeza halmashauri zote kutenga maeneo yenye miundombinu yote, ili kuondoa mivutano ya mara kwa mara kati yao na uongozi wa halmashauri hizo.

Lakini hadi leo wamachinga wanaendelea kuzagaa mitaani kufanya biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi, na wakati mwingine kufukuzwa, hali ambayo inaweza kukwamisha juhudi zao za kuchangia pato la taifa.

Wengine wanaendelea 'kuvamia' hifadhi za barabara kuchimba au kulima nyasi za kuweka vibanda bila kujali kwamba kitendo hicho kinaharibu mazingira na kusababisha mmomonyoko wa ardhi.

**Hata hivyo, wakati serikali ikitambua na kuthamini mchango wao katika kukuza pato la taifa, bado halmashauri hazijawawekea mazingira rafiki ya kufanyia biashara, hali inayosababisha wahangaike huku na kule kila mara.**

Inawezekana wanafanya hivyo kutokana na halmashauri zao kutowatengea maeneo ya kufanyia biashara, ingawa serikali kuu ilishaelekeza kundi hilo kujengewa masoko ya kufanyia biashara.

Halmashauri zinakwama wapi kutenga maeneo yenye miundombinu yote muhimu, ili wamachinga waondokane na mtindo wa sasa ambao unahatarisha maisha yao na pia kuharibu na kuchafua mazingira?

Kwa mfano, wamachinga wa Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam, wengi wao wameziba mitaro ya maji ya mvua, njia za waenda kwa miguu na pia kupanga bidhaa pembezoni mwa barabara ya Morogoro.

Ufanyaji biashara katika mazingira hayo unaweza kuhatarisha usalama wao, kwani wanaweza kugongwa na magari, kujeruhiwa lakini kuharibu na kuchafua mazingira ya Jiji la Dar es Salaam.

Si vibaya takwimu zilizotolewa na Waziri Mkuu kuhusu mchango wa wamachinga, zikawashutua viongozi wa halmashauri, ili waharakishe ujenzi wa masoko ya kutosha ambayo yatatumiwa na kundi hilo.

Zipo sababu mbalimbali zinazotolewa na wamachinga, ambazo zinawafanya wasihamie katika masoko yao ikiwamo kukosekana kwa miundombinu yote muhimu sokoni ikiwamo maji, vyoo na usafiri.

Ninaamini kwamba, ili kuimarisha uchumi wa wamachinga bila kuchafua mazingira ikiwamo kujisaidia ovyo, kuna haja ya kuwapo kwa huduma hizo muhimu kabla ya kuwahamisha.

Lakini wakati wakiandaliwa maeneo bora ya kufanyiwa biashara, si vibaya hata wenyewe wakajiongeza kwa kuepuka uchafuzi, uharibifu wa mazingira na kuhatarisha maisha yao, kutokana na kwamba ajali hazina hodi.

Ni vyema wakaachana na msemo wa 'tutakwenda wapi', kwani suala la usalama wao ni lao mwenyewe, hivyo ingefaa waangalie usalama wao kwanza, biashara baadaye, kuliko kuhatarisha maisha.

## Asakwa tuhuma za kutorosha dhahabu

**Na Mohab Dminic,** MBOGWE

JESHI la Polisi mkoani Geita linamsaka mmiliki wa leseni ya mgodi wa Kanegere unaosimamiwa na kikundi cha Isanjabadugu uliopo katika Kata ya Nyakafuru Wilaya ya Mbogwe, Warwa Katemi Warwa, kwa kosa la kutorosha mawe yanayodaiwa kuwa na madini ya dhahabu.

Tukio hilo lilitokea hivi karibuni katika Kata ya Nyakafuru, wilayani Mbogwe, mgodi wa Kanegere uliopo Kata ya Nyakafuru ambao unalalamikiwa kwa muda mrefu na wananchi wanaodai kudhulumiwa mashamba yao.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alikiri kuwapo kwa tukio hilo na kwamba gari lililojaa mawe yanayodaiwa kuwa na dhababu linashikiliwa.

Warwa anadaiwa kuhusika na utoroshaji huo wa mawe yenye madini ya dhahabu katika mgodi unaosimamiwa na kikundi cha Isanjabadugu ambacho yeye pia ni mwenyekiti.

Kikundi hicho kinalalamikiwa kwa muda mrefu na baadhi ya wananchi kwa madai ya kuvamia mashamba ya wananchi na kufanya shughuli za uchimbaji wa madini. Akizungumzia sakata hilo, Ofisa Madini wa kanda ambaye pia ni Kaimu Ofisa Madini mkoa wa kimadini wa Mbogwe, wilayani Geita, Joseph Kumburu, alisema tayari amemwandikia barua mmiliki huyo ajisalimishe katika Kituo cha Polisi Masumbwe.

Alisema hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 ili iwe fundisho kwa wachimbaji wengine ambao sio wazalendo.

Pia, alisema jalada la uchunguzi dhidi ya utoroshaji wa mawe ya dhahabu, MBG/RB/1275/2021 limefunguliwa.

Kumburu alisema katika ukaguzi maofisa wake walibaini upungufu ikiwamo kutokuwapo kwa alama za utambuzi wa mipaka kinyume na kifungu cha 52 (b) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017.

Upungufu mwingine ni kuwapo kwa maduara yaliyotelekezwa na wamiliki na kuwa hatarishi kwa usalama wa watu kinyume na kifungu cha 52 (c) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na kifungu cha 206 (1) (a) cha (kanuni ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira) 2018. Kutozingatia matumizi ya vikinga mwili (PPE) kwa wanaofanya shughuli za uchimbaji katika maduara yaliyopo katika eneo la leseni. Makosa mengine ni kushindwa kuwasilisha taarifa zinazoonyesha ulipaji wa mrabaha unaotokana na uzalishaji wa madini.

Pia, kushindwa kutoa taarifa ya ada ya mwaka ya leseni na taarifa za uzalishaji, kusimamia mpango wa utunzaji wa mazingira, kushindwa kusimamia utaratibu wa migao katika leseni yake na kusababisha kufanyika migao mingine baada ya maofisa wa serikali kumaliza usimamizi, kitendo kinachoashiria ukwepaji wa kodi za serikali.

Kwa upande wake mmiliki huyo, Warwa akizungumzia madai hayo, alisema ana mpango wa kukimbilia kwa Mkuu wa Wilaya Mbogwe ili amsaidie pamoja na wenzake.

Hata hivyo, alishindwa kutoa ufafanuzi kuhusu gari lililokamatwa na maofisa wa serikali likitorosha mawe yanayodaiwa kuwa na dhahabu.




Askari Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, akiangalia mzozo wa dereva wa daladala linalofanya safari zake kati ya Mbagala na Kawe na wa lori la mizigo, baada ya kugongana katika Barabara ya Kawawa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mbunge abanwa tozo miamala simu

**Na Thobias Mwanakatwe**

SUALA la tozo za miamala ya fedha kwenye simu sasa limehamia majimboni baada ya wananchi wa Jimbo la Ileje mkoani Songwe kumbana mbunge wao wakihoji ni kwa nini walipitisha suala hilo ambalo limekuwa kero kubwa kwao.

Mbunge wa Ileje, Injinia Godfrey Kasekenya, alikumbana na swali kuhusu tozo lililoulizwa na mwananchi Patrick Mchangilwa kwenye mkutano wa hadhara wakati akizungumza juzi na wananchi wa kata ya Ibaba wilayani Ileje.

"Mheshimiwa mbunge tozo ni kero kubwa, hatujazoea. Tunapata kero kubwa liangalieni suala hili, watu wa chini tunaumia," alisema huku akishangiliwa na wanakijiji wenzake.

Akijibu swali hilo, Kasekenya alisema tozo inayotolewa kwenye simu ipo kisheria na ni maalum kwa ajili ya kupata fedha kutatua changamoto za elimu, afya, maji na barabara.

"Tumesema hatuna wa kuwategemea. Barabara inayojengwa inajengwa kwa fedha za tozo na kimsingi wananchi wanacholalamika siyo tozo bali ni kwamba tozo ni kubwa," alisema.

Mbunge huyo alisema baada ya malalamiko ya wananchi kuhusu tozo ya miamala ya simu, Rais Samia Suluhu Hassani alishalichukua ili kuangalia namna ya kupunguza tozo na si kuondoa kwa sababu zipo kisheria.

Suala la wananchi kuendelea kupaza sauti limekuja huku Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kikiwa kimejitosa kwa kufungua kesi Mahakama Kuu.

LHRC imeshafungua shauri hilo namba 11 ya mwaka 2021 kuomba mapitio ya Mahakama Kuu kuhusu Sheria ya mfumo wa Malipo ya Taifa (National Payment System) Na. 437 pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari hivi karibuni, alisema kesi hiyo ambayo ipo kwa Jaji Irvin Mgeta, imeshatajwa kwa mara ya kwanza Agosti 5, mwaka huu, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Alisema LHRC imefungua kesi hiyo kutokana na kupitishwa kwa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali 2021/22 pamoja na Sheria ya Fedha ambayo ilisababisha kuweka tozo katika miamala ya fedha inayofanywa kwa njia ya simu. Henga alisema kufuatia tozo hiyo, limesababisha mzigo kwa wananchi wa kawaida pamoja na wafanyabiashara wadogo na wakubwa.

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaan, itasikiliza tena kesi hiyo kwa mara ya pili Agosti 16, mwaka huu.

## Waziri ataka ushirikishaji wadau mipango miji

**Na Munir Shemweta,** BABATI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kushirikisha wadau wa sekta mbalimbali wakati wa utekelezaji mpango kabambe katika maeneo yao.

Aidha, ametaka mipango ya kina inayoandaliwa katika halmashauri za miji na majiji kuzingatia mipango kabambe inayoandaliwa, ili kuifanya miji kuwa na taswira nzuri.

Dk. Mabula alisema hayo jana wilayani Babati Mkoa wa Manyara wakati akizindua Mpango Kabambe wa Mji wa Babati akiwa katika ziara ya siku moja ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi.

Alisema ni vizuri watendaji wa halmashauri kuhakikisha wakati wa utekelezaji mipango kabambe wanashirikisha wadau kama vile sekta za maji, barabara na umeme na kusisitiza kuwa hawatakiwi kwenda kinyume cha mambo yaliyowekwa katika mpango huo, ili kuifanya miji kuwa na taswira nzuri na inayovutia.

Naibu Waziri aliongeza kuwa wizara yake inaendelea kuhamasisha uandaaji mipango kabambe kwenye maeneo mengine nchini, ili kuongeza kasi ya upimaji pamoja na kuifanya miji kuwa katika sura nzuri.

"Kikubwa utekelezaji uzingatie mpango na lazima uwekwe wazi kwa kushirikisha wadau na kukabidhi kila mdau kipande chake cha utekelezaji. Mfano barabara TANROADS (Wakala wa Taifa wa Barabara) au TARURA (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini) akabidhiwe. Umeme akabidhiwe TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) na maji wapewe mamlaka za maji," alisema.

"Unakuta barabara nzuri halafu anakuja mtu wa maji anapitisha mabomba yake na anaharibu kabisa na hapa lengo ni kuona miji yote inapangwa vizuri," Naibu Waziri.

Dk. Mabula aliuelezea mpango kabambe aliouzindua kuwa njia mojawapo ya kutoa fursa za ajira sambamba na kuongeza kasi ya upimaji na hivyo kupunguza ama kuondoa migogoro ya ardhi.

Alizitaka halmashauri ambazo bado hazijaandaa mipango kabambe kuiga mfano wa Halmashauri ya Mji wa Babati kwa kuandaa mipango kabambe, ili kuchangia shughuli za kiuchumi. Pia aliagiza ofisi za mikoa na wilaya kufuatilia na kupatiwa ripoti ya utekelezaji Mpango Kabambe katika halmashauri husika, ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kimazingira.

Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Makazi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Imaculata Senje, alisema lengo la serikali katika uaandaaji mpango kabambe ni kuona kasi ya upangaji inaoongezeka.

Kwa mujibu wa Senje, hadi sasa mipango kabambe 30 imeandaliwa kwenye makao makuu ya wilaya nchini na kusisitiza kuwa mipango hiyo inapoandaliwa hushirikisha sekta zote muhimu kama vile barabara, maji na umeme.

# Bil. 35/- kutumika kujenga Uwanja wa Ndege Musoma

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inatarajia kutumia Sh. bilioni 35 kuboresha Uwanja wa Ndege wa Musoma, kwa kuweka lami na kuongeza urefu ili kuruhusu ndege kubwa na ndogo kutua.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi, Dk. Leonard Chamuriho, alisema hayo jana alipofika uwanjani hapo kukagua maandalizi ya ujenzi huo.

"Tunatarajia ujenzi huu utagharimu Sh. bilioni 35 ambazo zitahusisha upanuzi wa uwanja pia uwekaji wa lami. Naamini kazi hizi zikikamilika uwanja huu utakuwa wa kisasa zaidi," alisema. Waziri Chamuriho pia aliwataka wananchi wa mkoa huo ambao watapata ajira katika mradi huo, kuhakikisha wanatumia vizuri fursa watakayoipata kwa kuwa waaminifu na kufanya kazi kwa bidii.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Khalfani Haule, alisema mradi huo ukikamilika utarahisisha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Musoma na kuchochea biashara ya utalii kupitia Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo iko mkoani humo.

Aliongeza kuwa uongozi wa wilaya umejipanga kwa kuupokea mradi huo na kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa mkandarasi kwa kumpatia eneo la kuchimba mchanga na kokoto za ujenzi. Naye Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Musoma, Mohammed Bakari, alisema kazi ya ujenzi huo imepewa kampuni ya unjenzi ya Beijing kutoka China na itatumia miezi 20 kuanzia Aprili, mwaka huu na kukamilisha ifikapo Desemba mwakani.

Alifafanua kuwa mkandarasi huyo tayari ameshawasilisha vifaa vyake katika eneo la mradi kwa ajili ya kuanza rasmi ujenzi huo na kusisitiza kuwa ujenzi huo unasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mara.



Mhifadhi wa Hifadhi ya Misitu ya Amani Nature Reserve, Bob Matunda (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Unlock Amani' yenye lengo la kutangaza 'Amani Nature Reserve' iliyopo Tanga. Katikati ni mratibu wa mradi wa utunzaji wa vyanzo vya maji endelevu ya ardhi Tanga na Morogoro, Bakari Bamba na Mtaalamu wa Miradi ya Mazingira wa Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa UNDP, Abbas Kitogo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CRB yakopesha makandarasi hadi mil. 100/-

**Na Joseph Mwendapole,** MOROGORO

MFUKO wa kuendeleza makandarasi wazalendo Contractors Assistance Fund (CAF) chini ya Bodi ya Usajili wa makandarasi (CRB), umeendelea kuimarika na sasa umeshaanza kuwakopesha makandarasi hadi Sh. milioni 100.

Hayo yalisemwa jana mkoani hapa na Naibu Msajili wa CRB, Mhandisi David Jere, kwenye mkutano wa mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi.

Alisema CRB ilianzisha mfuko huo miaka ya hivi karibuni kwa ajili ya kuwakopesha makandarasi, ili kuanza kazi mara moja wanapopata miradi na walianza na Sh. milioni 50 tu.

"Kwa sasa mfuko wa makandarasi umeendelea kuimarika na una uwezo wa kuwakopesha kila mkandarasi mwanachama hadi Sh. milioni 100 kutoka Sh. milioni 50 za awali, hivyo hii ni fursa kwenu ukiwa na sifa unakopeshwa unaanza kazi mapema," alisema.

Pia alisema mfuko huo ulianzishwa kwaajili ya kuwawezesha makandarasi wazalendo kupata waranti ya malipo ya awali wanapopata miradi ya ujenzi na ulinzi wa zabuni wanazoomba.

Alisema CRB iliamua kuanzisha mfuko huo baada ya kubaini kwamba makandarasi wengi hasa wadogo na wakati hawana uwezo wa kupata fedha, kwaajili ya waranti ya malipo ya kazi za ujenzi na ulinzi wa zabuni hizo.

"Awali wakati unaanza huu mfuko ulikuwa unakopesha makandarasi wa baadhi ya madaraja, lakini umekuwa ukikua siku hadi siku hivyo kwa sasa unasaidia kukopesha makandarasi wazalendo wa madaraja yote ilimradi awe mwanachama wa mfuko huo," alisema Jerre.

Alisema kwa sasa wanaendesha mfuko huo kwa kushirikiana na benki moja na kwamba makandarasi wengi wameshanufaika nao kwa kukopa na kufanyia shughuli za ujenzi wa miradi.

Mmoja wa makandarasi hao, Raphael Ngonyani, alipongeza hatua ya bodi kuanza kukopesha makandarasi kwani wengi wao ni wadogo na walikuwa wakipata shida kuanza, wakipata kazi.

Alisema makandarasi wazalendo wengi wamekuwa wakikumbwa na changamoto ya mitaji hasa ya kuanzia miradi hivyo mfuko huo ni neema kwa makandarasi wazalendo.

"Changamoto yetu ya siku zote ni mitaji, unakuta unapata kazi lakini hata yale malipo ya awali ambayo ni kama waranti ya kupata kazi unakosa sasa naamini wengi wameshakopa na naishauri CRB waongeze ifike hadi 300," alisema

Aliwashauri pia makandarasi wanaokopeshwa kupitia mfuko huo kuwa waaminifu kwa kurejesha kwa wakati, ili wenzao nao waweze kunufaika na mikopo ya mfuko huo.

## Wananchi wahamasishwa kutembelea hifadhi za asili

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wameshauriwa kutembelea hifadhi za asili ikiwa ni sehemu ya kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kuongeza pato la utalii, badala ya kuwaachia Wazungu peke yao kufanya utalii katika maeneo hayo.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mhifadhi wa Amani Nature Reserve, Bob Matunda, wakati akizindua kampeni inayojulikana kama 'Unlock Amani' ambayo itafanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 27, mwaka huu.

Alisema kampeni hiyo inalenga kutangaza utalii wa misitu asili na kutunza vyanzo vya maji ili kuhakikisha misitu endelevu na upatikanaji wa maji.

"Kampeni hii pia inalenga kutumia juhudi za pamoja kuhakikisha hifadhi hiyo inafahamika zaidi kwa jamii zinazoizingira kufahamu majukumu yao katika matumizi endelevu ya ardhi," alisema.

Matunda alisema kilele cha kampeni hiyo ni safari maalum ya siku tatu ambayo ni wazi kwa watu wote kwenda kuzuru Amani na kujionea vivutio vilivyopo mkoani Tanga pamoja na kufahamu mikakati iliyowekwa.

"Tunataka kuhakikisha kuwa tunafanya kazi kwa karibu na serikali na wadau wengine katika kutunza vyanzo vya mito Zigi na Ruvu ili kuhakikisha Mji wa Tanga unakuwa na maji ya kutosha muda wote."

Matunda alisema mradi wa matumizi endelevu ya ardhi utasaidia kuboresha maisha ya watu wanaoishi karibu na vyanzo vya maji vya mito Zigi na Ruvu.

Naye Mratibu wa mradi wa kuhifadhi vyanzo vya maji Tanga na Morogoro kutoka Wizara ya Maji, Bakari Bamba, alisema suala hilo linahitajika ushirikiano baina ya taasisi za serikali, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuhakikisha ardhi inatumika vizuri, maji yanapatikana kwa uhakika kwa mji wa Tanga na wananchi wanakuwa na maisha bora zaidi.

Mtaalamu wa Miradi ya Mazingira wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Abbas Kitogo, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za matumizi endelevu ya ardhi kupitia mradi wa matumizi endelevu ya ardhi ili kuboresha na kutunza vyanzo vya maji, kutangaza utalii wa misitu asili na kuboresha maisha ya watu wanaoishi pembezoni mwa hifadhi ya Amani.

## Bosi mpya TADB aahidi matokeo

**Na Beatrice Moses**

MKURUGENZI Mtendaji mpya wa Benki ya Maendeleo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, ameanza kazi na kuahidi matokeo na kuwataka wafanyakazi wa benki hiyo kumpa ushirikiano.

Ameahidi pia kufanya kazi kiuweledi sambamba na kuleta mageuzi makubwa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi hapa nchini.

"Napenda kuona kila mfanyakazi anafanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya ili kufanikisha malengo ya benki ya kuleta mageuzi kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi," alisema Nyabundege.

Akizungumza na wafanyakazi waliomlaki kumkaribisha jijini Dar es Salaam jana kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe na Rais Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hiyo hivi karibuni, Nyabundege ambaye amebobea katika masuala ya benki na kifedha, alisema TADB ni chombo muhimu katika kuleta mapinduzi kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na hivyo amejipanga kuhakikisha benki hiyo itafikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa uundwaji wake.

"Nitahakikisha malengo yote yanatekelezwa kikamilifu sambamba na kuziwezesha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ziweze kutoa mchango stahiki katika kujenga uchumi wa nchi na kuongeza pato la taifa," alisema huku akishangiliwa na wafanyakazi waliokuwa wamejawa furaha na bashasha kubwa.

Alieleza kuwa TADB ina nafasi kubwa ya kupelekea mageuzi ya kiuchumi kupitia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuhakikisha wakulima wadogo wanapatiwa mikopo na elimu juu ya kuongeza tija katika uzalishaji na thamani ya mazao.Nyabundege alisema ni ukweli usiopingika kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wamejiajiri au kujihusisha moja kwa moja na shughuli za kilimo hivyo TADB ni lazima iwainue zaidi kwa kuwapa mikopo.

"Tija katika uzalishaji mazao itakapoongezeka itachochea uanzishwaji wa viwanda vingi vya kuchakata mazao na kupelekea ongezeko la ajira kwa vijana hali itakayosaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa ajira nchini," alisema Nyabundege.

Alisema usalama wa chakula nchini unategemea katika uzalishaji wenye tija hivyo TADB itaendeleza juhudi zake za kuhakikisha uzalishaji wa mazao unaongezeka na kuifanya nchi kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya kuuza nje ya nchi.

Katika hatua nyingine, alimshukuru Rais Samia kwa kumteua kuiongoza benki hiyo ambayo ina dhamana ya kutoa mikopo kwa wakulima na kuhakikisha mnyororo wa thamani wa mazao katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi unaboreshwa.

"Ni heshima kubwa kuteuliwa na kiongozi mkuu wa nchi hii ni hamasa kwangu katika kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kujitoa zaidi ili kufikia malengo ya serikali kwa kulifanya taifa letu kuwa katika uchumi wa viwanda," alisema.

Aidha, aliwataka watendaji wote katika benki hiyo muhimu kumpa ushirikiano ili kufikia malengo na faida ya kuwapo kwa benki hiyo ikawanufaishe wengi kwa kuhakikisha mageuzi makubwa yanafanyika katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Kabla ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo, Nyabundege alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Lake Oil Tanzania Limited na vilevile ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika sekta za kibenki. Aliwahi pia kuhudumu kama Mkurugenzi Mtendaji wa TIB Corporate Bank Tanzania Limited.

# Kampeni elimu kwa mlipakodi yawavutia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI ya usajili wa walipakodi wapya inayoendelea katika maeneo ya Ilala, Kinondoni, Kigamboni, Kariakoo na Temeke mkoani Dar es Salaam, imewavutia wafanyabiashara wapya ambao walikuwa hawajasajiliwa katika mfumo wa kodi.

Kampeni hiyo inayoendeshwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuitaka TRA kuongeza wigo wa walipakodi nchini.

Mlenzi Selemani, msimamizi wa kampeni hiyo katika Wilaya ya Temeke, alisema TRA imeamua kuwasogezea huduma karibu walipakodi na mwitikio umekuwa mkubwa.

"Pamoja na kutekeleza agizo la Rais, tumeamua kutoka kwenye ofisi zetu ili kusogeza huduma karibu na wafanyabiashara ambao wengine wanashindwa kuja ofisini kutokana na changamoto mbalimbali. Tunashukuru watu wamejitokeza na kusajiliwa kuwa walipakodi," alisema.

Selemani aliwahimiza wafanyabiashara wote wapya kutembelea vituo vilivyowekwa maeneo mbalimbali Dar es Salaam ili kupata huduma ya kusajiliwa na kupatiwa cheti cha Utambulisho wa Mlipakodi (TIN).

"Ninachukua fursa hii kutoa wito kwa wafanyabiashara wapya kuendelea kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vilivyowekwa katika maeneo ya Ilala, Kinondoni, Kigamboni, Kariakoo na Temeke ili wasajiliwe na kupatiwa TIN," alisema.

Mfanyabiashara kutoka Temeke, Rukia Ganya, aliishukuru TRA kwa kumwelimisha masuala mbalimbali yanayohusu kodi ikiwa ni pamoja na kumsajili kuwa mlipakodi.

"Ninaishukuru TRA kwa kuleta kituo cha usajili hapa Temeke, mimi ni mfanyabiashara mpya na sikujua kama ninatakiwa kuwa na TIN, lakini maofisa wa TRA wamenielimisha na nimesajiliwa rasmi kuwa mlipakodi," alisema.

Mfanyabiashara wa Tandika Sokoni, Manga Bakar, alisema TRA kuweka vituo vya usajili katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, kumerahisisha kuokoa muda wa kuwafuata ofisini kwa kuwa wakati mwingine kunakuwa na foleni kubwa ya wateja wanaotaka huduma.

Kampeni hii ya usajili wa walipakodi wapya ni endelevu na kwa Dar es Salaam inatarajiwa kumalizika Agosti 31, mwaka huu na kuelekezwa mikoa mbalimbali nchini.

Ilizinduliwa rasmi Agosti 5, mwaka huu na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amosi Makalla, ikiwa na lengo la kuongeza wigo wa walipakodi na kuongeza makusanyo ya serikali.




Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA), Mkoa wa Geita, Moses Ntungi (kulia) na Ofisa Vipimo, Festo Robert, wakitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo katika maonyesho ya kuhamasisha utalii na biashara wilayani Chato, mkoani humo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana waonyeshwa fursa usafiri mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za usafiri mtandaoni kwa kuwa utawasaidia kupata ajira ya uhakika.

Ushauri huo umetolewa na Fabian Shao (32), ambaye amesema kuwa baada ya kuacha kazi ya udereva katika shirika moja la kimataifa na kuamua kujiajiri na kuwa dereva wa Bolt, amepata mafanikio makubwa katika maisha yake.

Shao, ambaye ni mkazi wa Chanika Dar es Salaam mwenye mke na watoto watatu, amesema kuwa amefanya kazi na shirika moja ambalo hakutaka liandikwe kwa miaka miwili, lakini baada ya kuingia bolt amepata mafanikio makubwa pamoja na kuwa mjasiriamali kwa kufungua biashara.

Anaeleza kuwa hakuwa rahisi uamuzi aliochukua wa kuacha kazi pamoja na uamuzi wa kuchukua mkopo wa gari wa riba nafuu kwani mke wake hakuamini kuwa angeweza kufanikiwa.

Shao alisema kuwa kilichomsukuma kuchukua mkopo ni kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu bila mkataba wa kidumu huku mshahara anaolipwa kutokidhi mahitaji yake na kushindwa kutimiza malengo yake.

Alisema ilifika wakati, kuwalipia ada watoto wake ambao mmoja anasoma kidato cha kwanza na wa pili darasa la tano na watatu darasa la tatu ilikuwa ngumu, kutokana na kipato kidogo na kukosa chanzo kingine cha mapato.

"Nilikuwa nafanya kazi katika shirika moja kubwa tu hapa Dar es Salaam, kama dereva, nimefanya kwa miaka miwili bila kuona nikisogea kimaendeleo ndipo nilipoamua kuacha kazi na kuchukua mkopo na kununua gari kwa ajili ya Bolt," alisema na kuongeza:

"Niliweka malengo na nimefanikiwa, ndani ya mwaka mmoja nimemaliza mkopo, na kwa sasa nimenunua gari nyingine, watoto wangu wana uhakika wa kusoma, nimefungua sehemu ya kuosha magari (car wash) na nimempa mtaji mke wangu wa kufuga kuku wa kisasa, kwa kweli najivunia sana kuwa dereva wa Bolt."

Amewapa ushauri vijana kufanya kazi ya usafiri mtandaoni na Bolt kwani ni kampuni ambayo inawasaidia vijana kujikwamua katika maisha pamoja na kutimiza malengo yao.

# Wakulima 17 kortini tuhuma za vurugu

**Na Saud Hamdan,** LINDI

WAKULIMA 17 katika vijiji vya wilaya za Ruangwa na Kilwa, mkoani Lindi wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka manne.

Miongoni mwa mashtaka hayo ni uvunjifu wa amani, kuharibu mali za umma na kusababisha hasara ya shilingi 4,800,000.

Walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Lindi, huku wakidaiwa kutenda kosa hilo Julai 25, mwaka huu majira ya mchana.

Walisomewa mashtaka hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Maria Betraine na Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo.

Waliofikishwa mahakamani ni Ramadhani Hamisi (43), mkazi na mkulima wa kijiji cha Chienjere Wilaya ya Ruangwa; Mwarami Kassimu Mbepei (42); Chande Abdallah Mtumba (40); Juma Hashimu Mkaindo (42); Omari Rashidi Lipau (38); Chande Ally Lipenga (25) na Salum Ally Lipita (26).

Wengine ni Halifa Abdallah Mpambayage (25); Abdukarimu Muhindi (35); Saidi Ally Mnyuve (31); Mohamedi Nassoro Nandonde (30); Mohamedi Abdull Lipenga (25); Rajabu Maulidi Mbepei (23); Abdallah Salum Mpacho (32); Kassimu Hemedi Mkwanga (42); Selemani Rashidi Selemani (42) na Hamza Mussa Mbepei (27), wakazi Kijiji cha Mtepera, Kilwa.

Gumbo alidai kosa la kwanza la kufanya vurugu zilizosababisha kutoweka kwa amani chini ya kifungu cha 89 (1) (b) cha Sheria ya adhabu ya makosa ya jinai, kosa la pili kushindwa kutii amri halali ya Jeshi la Polisi.

Kosa la tatu kuzuia kutumika njia ya umma kinyume cha kifungu cha 239 na kosa la nne kufanya uharibifu wa mali za umma, yakiwamo magari mawili ya serikali. Magari hayo ni Toyota Landcruser STL 6246 na STL 8136 na kusababisha hasara ya jumla ya Sh. 4,800,000.

Hata hivyo washtakiwa walikana makosa na kupelekwa rumande, kutokana na wadhamini wao kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, na kesi hiyo namba 07/2021 itatajwa tena Agosti 24, mwaka huu.



Dereva wa bodaboda akipita kwenye barabara ya mabasi ya mwendokasi, eneo la Msimbazi Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DC aja juu wenye ulemavu kuonewa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amepiga marufuku watu wenye ulemavu kukatwa fedha za mikopo wanazoomba kupitia fedha za ndani za halmashauri.

Fedha hizo ni asilimia 10, ambazo watu wenye ulemavu wanapata asilimia mbili, wanawake asilimia nne na vijana asilimia nne.

Mboneko alibainisha hayo jana wakati akikagua mradi wa nguruwe, ambao unatekelezwa na watu wenye ulemavu Kitangili katika Manispaa ya Shinyanga, akiwa ameambatana na kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini.

Alisema baada ya kusikia taarifa ya watu hao wenye ulemavu kulalamikia kukatwa fedha za mikopo kiwango ambacho wanaomba halmashauri na kupewa fedha nusu, aliagiza wasikatwe.

"Naagiza kuanzia sasa ni marufuku watu wenye ulemavu kukatwa fedha za mikopo asilimia mbili ambazo wanaomba, wapewe kiwango sahihi, sababu ni kundi maalumu na wapo wachache, na mkikatwa tena fedha zenu nipeni taarifa," alisema Mboneko.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Abubakari Mukadam, ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa kutoa fedha za mikopo kwa watu wenye ulemavu, kwa lengo la kuwainua kiuchumi kwa sababu kundi hilo huwa linasahaulika.

Awali mwekahazina wa kikundi hicho cha watu wenye ulemavu, Janety Maganga, akisoma taarifa, alisema kikundi chao kina watu wanne wanaojihusisha na ufugaji wa nguruwe, na waliomba fedha za mikopo Sh. milioni 5, lakini walipewa Sh. milioni 3, fedha ambazo wamedai kutokidhi mahitaji yao.

# Daraja la Nyamwifa kulamba mil. 300/-

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya Sh. milioni 300 zitatumika kujenga upya daraja la Mto Nyamwifa katika Kijiji cha Bugunda, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, lililoharibika miaka mitatu iliyopita.

Kuharibika kwa daraja hilo kulikwamisha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) wilaya hiyo, Mhandisi Hussein Abbas, alisema jana kuwa fedha hizo zimetolewa na mfuko wa barabara na mkandarasi yuko kwenye eneo la kazi.

"Daraja la Nyamwifa liliharibika tangu mwaka 2018 na kusababisha magari kushindwa kupita na, hivyo kukwamishwa shughuli mbalimbali za maendeleo, lakini sasa tatizo hilo litakwisha," alisema Mhandisi Abbas.

Alifafanua fedha za mfuko wa barabara, zitatumika katika ujenzi wa daraja hilo, ulimaji wa barabara ya kilomita 5.0, uwekaji wa makalavati matatu, uchimbaji wa mitaro na uwekaji wa kifusi sehemu korofi.

"Mkandarasi M/s Flow Services and Supplies Ltd, alisaini mkataba wa ujenzi Julai mwaka huu na tumekubaliana awe amekamilisha kazi Oktoba mwaka huu kabla ya mvua za vuli hazijaanza kunyesha," alisema.

Alisema, serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara za Musoma Vijijini, likiwamo daraja la Nyamwifa ambalo linaunganisha vijiji mbalimbali vya kata za Bulinga, Bwasi na Bukima.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Bwasi, Mashaka Kagere, alisema, daraja hilo liliharibika na kusababisha shughuli za kijamii kuzorota, ikiwamo magari ya kusafirisha samaki kutoka Kome Beach kushindwa kusafirisha biashara hiyo.

Aidha, Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, ameishukuru serikali kwa kutenga Sh. bilioni 2.85 katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya uboreshaji wa barabara jimboni humo.

"Mawasiliano ya barabara hufungua shughuli nyingi zikiwamo za kiuchumi, hivyo kwa niaba ya wananchi wa Musoma Vijijini, ninaishukuru serikali kwa kutenga fedha hizi kwa ajili ya barabara zetu," Prof. Muhongo alisema.

Alisema, wakazi wa jimbo hilo wanajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara na kwamba uboreshaji wa barabara utarahisisha pia usafirishaji wa mazao kwenda sokoni.

# Hospitali ya Njombe yamsikitisha Ummy

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesikitishwa na hali ya Hospitali ya Halmashauri ya Njombe kuhudumia wagonjwa watatu kwa siku na kusema ni matumizi mabaya ya rasilimali.

Waziri alieleza masikitiko yake hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea hospitali hiyo iliyojengwa Kijiji cha Matembwe ambapo alisema kuna zahanati kwa siku zinaona wagonjwa hadi 200.

"Sasa hospitali ambayo ni halmashauri inatakiwa kuwa kubwa, lakini inaona wagonjwa watatu kwa hiyo sioni matumizi mazuri ya rasilimali, mganga mkuu wa hapa anasema watu wanahitaji huduma, lakini hawaji kwa sababu hakuna vifaa tiba hili nalibeba niwaahidi wana-Njombe nitalifanyia kazi.

Pia Waziri Ummy aliwataka wakurugenzi nchini kuwa makini kwa kuangalia maeneo ya kuweka miundombinu ya kutoa huduma kwa wananchi.



Ukurasa 14

Umemejua unavyokoleza uwekezaji vijijini, shuleni



Ukurasa 13

Siasa za Bongo ziwe sawa na Simba, Yanga



Ukurasa 12

**KUOZA MATUNDA, MBOGA**

**Wakulima, wafanyabiashara wataka viwanda na miundombinu kuhifadhi**

BUFE


IJUMAA AGOSTI 13, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# CPB inapowatangazia neema walima mahindi

**Na Beatrice Philemon**



Wafanyabiashara wa mahindi wakiwa sokoni Kibaigwa mkoani Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

WAKULIMA wa mahindi waliokuwa wanapunjwa wamepata mkombozi, baada ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), kutangaza kununua zao hilo kwa Shilingi 500, katika maeneo ambayo walikuwa wanauza kwa bei ya chini.

Ni mambo yanayotokea katika mikoa iliyokuwa ikiuza mahindi kwa bei ndogo na kusababisha wakulima kukata tamaa ya kilimo hicho.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CPB, Dk. Anselm Moshi, anasema katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa bei hiyo elekezi ni agizo la serikali na itaanza kuwanufaisha wakulima wa mahindi Mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe, Songea , Dodoma, Manyara na Arusha.

Dokta Moshi anasema baada ya kupata agizo kutoka kwa serikali walitakiwa kununua mahindi katika mikoa hiyo, ili kunusuru wakulima ambao waliuza mazao kwa bei ya chini akitaja Shilingi 150 na wengine 175.

Anaongeza kuwa hata hivyo kasi ya ununuzi ilikuwa ndogo kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha unyevu katika mahindi yao, kazi iliyoanza Juni mwaka huu..

"Ili kusaidia wakulima kuuza mahindi yao kwa bei nzuri, bodi ilifungua vituo vya muda vya kuyanunua ambapo katika Mkoa wa Katavi Wilaya ya Mlele vipo vituo 10 katika eneo la Majimoto, Kashishi, Manela, Mirumba, Mbede, Itura, Kibaoni, Kavuu, Usevya na Chamaland," anasema Dk. Moshi.

Katika vituo hivyo tani 1,000 za mahindi zilinunuliwa katika maeneo hayo na kazi inaendelea.

Anaeleza kuwa vituo vingine vimefunguliwa katika Wilaya ya Tanganyika na mahindi katika Mkoa wa Katavi yanannunuliwa kwa wastani wa Shilingi 280, kwa kilo moja lakini CPB inanunua kwa Shilingi 500.

**UNUNUZI RUVUMA**

Akizungumzia hali katika Mkoa wa Ruvuma, anasema ununuzi wa mahindi umeanza mwezi uliopita katika vituo vya Songea mjini na Kigonsera, na tayari tani 810 zimenunuliwa .

"Ununuzi katika Wilaya ya Nkasi umeanza rasmi Julai 21 mwaka huu, kwa sasa bei ya mahindi kwenye Wilaya hiyo ilikuwa kati ya Shilingi 250 hadi 270 kwa kilo," anasema Mtendaji Mkuu.

Mkoa wa Songwe na maeneo ya Sumbawanga tani 10,823 za mahindi zimenunuliwa kupitia wafanyabiashara wa kati wanaoyachukua kwa wakulima na kuiuzia Bodi ya CPB.

Na katika vihenge vilivyoko Mkoa wa Iringa anasema tani 8,900 zimenunuliwa kwa bei ya Shilingi 430 kwa kilo wakati Dodoma tani 1,920 za mahindi zimeuzwa kwa bei ya Shilingi 450.

**TANI 144,000 KWENDA MOMBASA**

Anasema hadi sasa bodi imetumia Shilingi bilioni 7.47 kununua tani 14,948, kwa wastani wa Shilingi 500 kwa kilo akieleza kuwa mipango ya ununuzi wa mwaka 2021/2022 lengo ni kununua tani 298,000, licha ya mazao mengine kama mtama, mpunga, maharage na alizeti kukusudiwa pia.

"Hii ni kutokana na uwepo wa mikataba miwili mikubwa pamoja na malighafi, kwa ajili ya kiwanda chetu," anasema Dk. Moshi.

Anaeleza kuwa bodi inamkataba na kampuni ya Grain Industries Ltd ya Mombasa kwa ajili ya kuwauzia tani 144,000 za mahindi zenye thamani ya Shilingi bilioni 7.5, na tayari tani 1,000 zimeshasafirishwa na kila mwezi bodi itakuwa ikipeleka tani 12,000 Mombasa.

**BODI INAILENGA WFP**

Mbali na hilo, mazungumzo kati ya bodi ya mazao mchanganyiko na Mpango wa Chakula (WFP) wa Umoja wa Mataifa, yanaelekea kukamilika, ili kuiuzia WFP tani 50,000 za mahindi.

Pia bodi kwa kushirikiana na kampuni ya Kapari Limited ya Dar es Salaam, inayomilikiwa na rai wa Kenya wapo katika hatua za mwisho kufungua ghala la kuhifadhi tani 102,000 za mahindi katika jijini Nairobi .

"Mahitaji ya viwanda vya CPB vya kusaga mahindi katika Mkoa wa Arusha, Iringa na Dodoma ni tani 54,000 za mahindi kwa mwaka," anasema Dk. Moshi.

Militon Lupa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Chakula wa Serikali (NFRA) anasema wanatarajia kununua tani 165,000 zenye thamani ya Shilingi bilioni 14 katika awamu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22.

Anasema watanunua mahindi kulingana na bei ya soko, lakini watakuwa wanunuzi wa bei ya juu, ili kutii agizo la serikali la kuwasaidia wakulima badala ya kuwapunja kwa kuwapa bei ndogo.

"Tutanunua kwa bei rafiki, ili wapate fedha za kujikimu na kuendelea na uzalishaji misimo ijayo. Hizi ni fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu na kwamba taasisi inasubiri kukabidhiwa fedha, ili kununua mahindi mikoa yenye bei ya chini."

Lupa anataja baadhi ya mikoa watakayonunua mahindi kuwa ni Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi ambako baada ya utafiti wamegundua wafanyabiashara wananunua kilo ya mahindi kwa Shilingi 150 hadi 175 wakati wengine hununua kwa Shilingi 280 hadi 400 kwa kilo.

Hata hivyo kazi hiyo itaanza wakati wowote baada ya serikali kuwapatia fedha.

UCHUMI

# KUOZA MATUNDA, MBOGA

## • Wakulima, wafanyabiashara wataka viwanda na miundombinu kuhifadhi

**Na Sabato Kasika**



Wadau wanatamani nyanya kama hizi, matunda kuwa na soko la uhakika na kuwapo kwa viwanda vingi vya kuyachakata. **PICHA: MTANDAO**

KILIMO ni uti wa mgongo wa taifa, ni kaulimbiu iliyoanza kutumika nchini tangu taifa lilipopata uhuru 1961, ikilenga kuweka na kuimarisha mikakati mbalimbali ya kukiendeleza, kwa ajili ya kujenga uchumi wa taifa na kuharakisha maendeleo ya nchi na mtu mmoja mmoja.

Hivyo, Watanzania hawawezi kukwepa kilimo kiwe cha matunda, nafaka, mboga, mazao ya biashara na viungo kutokana na ukweli kwamba, zaidi ya asilimia 60, wameajiriwa katika sekta hiyo ambayo, pia inahusisha ufugaji.

Hata hivyo, bado kilimo kinakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo ya ukosefu wa masoko ya uhakika na hata yaliyokuwapo hayawezi kununua bidhaa na kumlipa mkulima gharama alizotumia kwenye uzalishaji .

Lakini viwanda vya kuchakata mazao navyo havipo, hali inayosababisha baadhi ya mazao na matunda kuharibika au kuoza.

Wakulima wa matunda na nyanya, ni miongoni mwa wale wanaokumbwa na tatizo hilo hivyo ni jukumu la serikali na sekta binafsi kuwasaidia kupata soko na kuwahimiza walime kwa wingi matunda.

Ahadi ya serikali inatolewa kwa wakulima wa maparachichi, kwamba, inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Afrika Kusini, ili kupata soko la matunda hayo yanayolimwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema, hatua hizo zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zitasaidia kutatua kero ya wananchi kuingia hasara kwa kutupa matunda hayo baada ya kuoza, kutokana na kukosa soko.

Ni katika ziara yake wilayani Rungwe mkoani Mbeya baada ya kutembelea mashamba ya kiwanda cha maparachichi cha Kampuni ya Kuza Afrika Ltd kilichopo katika Kijiji cha Ilolo, Kata ya Kiwira. Majaliwa pia anawataka wakazi wa Wilaya hiyo na maeneo mengine ambayo zao hilo linastawi kwa wingi, kuendelea kuzalisha zaidi, kwa kuwa soko la uhakika litapatikana.

Wakati Waziri Mkuu Majaliwa akitoa ahadi hiyo, wadau na wakulima wa matunda nao wanashauri serikali njia nyingine zaidi, ambayo wanaamini inaweza kumalizaa kero ambazo wakulima hao wamekuwa wakikumbana nazo.

### VINAHITAJIKA VIWANDA

Pamoja na ahadi hiyo ya serikali, wanaamini kuwa ujenzi wa viwanda vidogo vingi nchini, unaweza kuokoa matunda na mboga visioze, kwa kuwa watakuwa na uhakika wa kwenda kuuza kuliko ilivyo sasa.

> **"Watu wengi huwa wananifahamu kwenye siasa, lakini mimi pia ni mkulima wa mazao mbalimbali na matunda, hivyo ninajua hali halisi ambayo wakulima wenzangu wanakutana nayo.**

Thomas Ngawaiya ni mkulima wa mihogo na matunda yakiwamo maembe na machungwa, anayeeleza kuwa mashamba yake yapo Handeni mkoani Tanga, anasema matunda mengi ya wakulima yanaoza kutokana na kukosa soko na viwanda vya kuyachakata.

"Ninaishukuru serikali kwa kuona shida ya wakulima wa maparachichi na kuwatafutia soko. Isiishie huko, bali hata matunda mengine, lakini zaidi ijenge viwanda vidogo vya kutosha vya kuchakata matunda," anasema Ngawaiya.

Anasema, miaka ya nyuma kulikuwa na taarifa za mara kwa mara, kwenye vyombo vya habari zikielezea jinsi wakulima wa nyanya wanavyotelekeza mashamba yao kutokana na kukosa soko na wanunuzi wa zao hilo.

"Ukielekea Mikoa ya Kaskazini, hasa msimu wa matunda, utashuhudia jinsi yanavyoharibika kuanzia maembe, mananasi na machungwa kwa kukosa soko, kama vingekuwapo vya kutosha wakulima wangeuza huko," anasema Ngawaiya.

Mkulima huyo anasema, umefika wakati sasa serikali kukaribisha wawekezaji wengi wajenge viwanda vya kutosha kuchakata matunda, ili wakulima waepuke hasara ya kila mwaka ambayo wamekuwa wakiipata.

"Watu wengi huwa wananifahamu kwenye siasa, lakini mimi pia ni mkulima wa mazao mbalimbali na matunda, hivyo ninajua hali halisi ambayo wakulima wenzangu wanakutana nayo," anasema.

Mkulima huyo anasema, mtazamo wake ni kuwapo kwa viwanda vingi vya kuchakata matunda nchini kama suluhisho la hasara ya miaka nenda miaka rudi ambayo wakulima wa matunda wamekuwa wakiipata.

### MAZOEA NI TABU

Muuza nyanya na matunda jijini Dar es Salaam Nyemo Juma, anasema, kufanya kilimo na biashara kwa mazoea, kumesababisha wakulima waone kama jambo la kawaida na kumbe wanaumia.

"Mfumo wa kilimo chetu unakabiliwa na changamoto nyingi. Kwa mfano, mkulima analima ekari tatu za nyanya kwa kutegemea muuza genge, katika mazingira kama hayo hawezi kupiga hatua kwenda mbele," anasema Nyemo.

Anasema, wakulima wa nyanya na matunda pamoja na wauzaji, ni kama wanaona ni jambo la kawaida kuozewa na bidhaa zao na kupata hasara, bila kutafakari na kuchukua hatua za kuwasaidia kuepuka hali hiyo.

"Imekuwa ni jambo la kawaida kukuta mkulima na mfanyabiashara anaozewa na rundo la nyanya au matunda kana kwamba ni sawa, lakini ingependeza iwapo wote wangepaza sauti ya kutaka viwanda, ili wauze huko," anasema.

Anasema, viwanda vingi vinasaidia kumfanya mkulima na mfanyabiashara kuwa na uhakika wa soko na siyo kuendelea kulima na kufanya biashara kwa mazoea, bila kujali hasara na muda wanaopoteza.

### KIWANDA KILA MKOA

Muuza nafaka katika soko la Tandale Dar es Salaam, Abdul Kambaya, anasema, umefika wakati sasa kujenga angalau kiwanda kimoja kila mkoa ambao unazalisha matunda kwa wingi.

"Ninasema hivyo, kwa sababu ninashuhudia jinsi ambavyo wafanyabiashara wa sokoni kwetu wanavyopata hasara kutokana na matunda, nyanya na bidhaa nyingine kuoza kwa kukosa soko,"anasema Kambaya.

Anasema, hata wafanyabiashara wanaonunua matunda mikoani na kupeleka katika viwanda vya Dar es Salaam, hukumbana na changamoto ya kukaa katika foleni kwa muda mrefu na matokeo yake yanaoza kabla ya kuuza.

"Hii yote inatokana na kutegemea kuuza sehemu moja, lakini kama kungekuwa na kiwanda japo kimoja kila mkoa, wakulima na wafanyabiashara wangekumbana na changamoto hiyo," anasema.

Kambaya anasema, hatua hiyo ingesaidia wakulima na wafanyabiashara kukamata soko la ndani na hata la nje kwa nchi jirani ambazo zinategemea matunda kutoka Tanzania.

"Lengo la serikali ni kufikia nchi ya viwanda, njia mojawapo ya kufikia hapo ni kuanza kwa viwanda vidogo, kwa ajili ya wakulima na wafanyabiashara wa matunda, kwani ndiyo wanapata shida ya kuozewa mazaoa yao," anasema.

Anasema, imani yake ni kwamba, kuwapo kwa viwanda vingi vya kuchakata matunda nchini, kutachochea na kuwapa hamasa wakulima kuongeza juhudi katika kilimo, kwa kuwa watakuwa na uhakika wa soko.

"Kimsingi, kuwapo viwanda vingi vya kuchakata matunda, kutasaidia juhudi za serikali za kutaka Tanzania kuingia kwenye masoko ya kimataifa kwa kuuza bidhaa zinazotokana na matunda yanayopatikana nchini," anasema.

Mfanyabiashara huyo anasema, Tanzania inaelezwa kuwa ni maskini kwa kuwa kilimo ambacho Mtanzania anakiendesha ni cha kukidhi mahitaji yake ya chakula na kama inakuwepo ziada inakuwa ni kidogo ambayo huiuza.

"Kilimo hicho kimepitwa na wakati, kwani hakilengi kumkomboa mkulima, hivyo ni muhimu kupiga hatua kwa kuwezesha wakulima na wafanyabiashara kupata soko la uhakika, ili kuepuka hasara zisizo za lazima," anasema..

Anasema, kilimo ni utajiri mkubwa iwapo nguvu kubwa itaelekezwa huko, kwa kuzingatia kuwa ndicho uti wa mgongo wa taifa na mkombozi wa Watanzania kiuchumi, hasa kukiwa na soko la uhakika.

"Asilimia kubwa ya wakulima, wanaishi vijijini, huku sekta hiyo ikikabiliwa na kero nyingi ikiwamo ukosefu wa zana bora za kilimo, upungufu wa wataalamu, ukosefu wa masoko ya mazao na migogoro ya ardhi," anasema.

Kambaya anasema, hayo yote yanatakiwa kupatiwa ufumbuzi, ili wakulima waweze kufaidi jasho lao kikamilifu badala ya kuendelea kuwa na maisha duni wakati wakizalisha mali mashambani.

### WANAOLIMA MBOGA WALIA

Mkulima wa mboga kutoka Mpwapwa, Elius Kange, anasema tatizo la kukosa miundombinu ya kuhifadhi mboga ni changamoto kwa wakulima. Anaeleza kuwa wakulima kila siku wanalazimika kufunganya mboga na kuzipeleka sokoni, wakati kama kungekuwa na miundombinu hiyo wangezihifadhi na kuuza wakiwa masokoni.

"Tunaomba kuwe na 'cold rooms au facilities ' za kuhifadhi mboga. Zijengwe masokoni au sehemu ambazo Halmashauri na serikali zitaona inafaa kuliko kuacha hali ibaki kama ilivyo. Kila siku wakulima wa Ruvu, Dodoma na kwingineko ni lazima walete mzigo wa mboga sokoni," anasema Kange.

Anakumbusha kuwa mboga zinahitaji kuhifadhiwa, ili wasiendelee kulima kizamani. Anasema katika kuzisafirisha zinaoza, zinaharibika na zinapofika sokoni zikikosa wateja haziwezi kuhifadhiwa badala yake hutupwa na mkulima kupata hasara.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Siasa za Bongo ziwe sawa na Simba, Yanga






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

TANZANIA kuna timu kuu mbili za soka, Simba na Yanga. Timu hizi huitana watani wa jadi, na zimekuwa zikipokezana ubingwa wa nchi tangu miaka ya thelathini zilipoanzishwa, huku mara moja moja sana zikipokwa na timu ndogo za mikoani.

Timu hizi zimesajiliwa na ni halali, zikiongozwa na sheria na kanuni za kusimamia soka nchini, chini ya Shirikisho la Vyama ya Soka Nchini (TFF), ambalo ndilo baba na mama wa soka likiwa na uamuzi wa mwisho, katika masuala yanayohusu mchezo huo.

TFF nayo ina wakubwa zake, ambao ni Shirikisho la Soka la Afrika (CAF) na Shirikisho la Kimataifa la Soka (FIFA) ambalo ndilo mama na baba wa mchezo huo pendwa duniani, wenye mashabiki wengi kuliko michezo yote.

Simba na Yanga, kama zilivyo timu zingine nchini, barani Afrika na duniani kote, kila mwaka baadhi yao hushiriki mashindano mbalimbali, makubwa yakiwa ni ligi za nchi husika, hivyo hukaa chini na kusajili wachezaji wapya.

Yote hayo husimamiwa na vyama vya soka katika nchi hizo na hatimaye majina huonekana CAF na FIFA, kwa ajili ya ufuatiliaji, pia kuhakikisha kuwa taratibu, kanuni na sheria zinazosimamia mchezo huo zinafuatwa.

Wakati wa kusajili, timu hizo hupewa muda wa kujiandaa, ili wachezaji wapya na wenyeji wazoeane na kujiandaa kwa msimu mwingine wa mashindano ya ligi za kitaifa na kimataifa, hasa kwa zile zinazokuwa zimefaulu kushiriki mashindano hayo ya kimataifa.

Hakuna wakati katika nchi, ambapo timu bingwa huzuia timu zingine kusajili, pia kufanya mazoezi na kujipanga kwa ajili ya michuano iliyo kwenye ratiba au hata michezo ya kirafiki ya kitaifa na kimataifa.

Endapo itatokea timu bingwa kuzuia timu nyingine kufanya mazoezi au kusajili wachezaji, na kutaka wakati wa ligi ndipo ziingie kushindana na mabingwa, ambao hujipa muda wa mazoezi na kusajili, bila shaka hakutakuwa na usawa katika mapambano.

Kumbe soka ni sawa na siasa katika jamii. Kwamba timu katika jamii ni vyama vya siasa, ambavyo huundwa kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanashiriki siasa, kwa maslahi yao na mustakabadhi wa maisha yao.

Hutokea vyama hivyo vikatofautiana kiitikadi, na ndipo hapo husababisha mgawanyiko wa timu bingwa; ambayo ni chama tawala kilichoshinda katika uchaguzi, na timu zingine ambazo ni vyama pinzani vinavyokuwapo kuhakikisha siku moja timu bingwa anakuwa mshiriki, baada ya kupatikana bingwa mwingine.

Nchini kwetu, tangu miaka mitano na ushei iliyopita na hata sasa, timu bingwa imekuwa ikizuia timu zingine kufanya mazoezi, hivyo hizi zingine zisubiri tu ligi bila kwenda uwanjani kujinoa.

Lengo la chama chochote cha siasa ni kutwaa madaraka ya nchi, kwa njia halali ambayo ni kwa kufanya uchaguzi.

Inakuwaje mathalan, kuiambia Yanga kwamba kwa kuwa Simba ndiye bingwa wa nchi, basi acheni kufanya mazoezi na badala yake benchi lenu la ufundi, lihamie Msimbazi, ili kusaidia kuinoa Simba, lakini ukifika wakati wa ligi rudini kwenu, ili mje tupambane! Inakuja kweli?

Sheria ya nchi inataka vyama vya siasa kupewa fursa kujijenga kisiasa, kujijenga ni pamoja na kukutana na kuelezana yanayotakiwa katika chama yanayohusu siasa ikiwa ni pamoja na kusajili wanachama wapya na kuchagua viongozi.

Kujiimarisha kichama ni pamoja na kuelezana sera na misimamo ya chama, pia mbinu za kuhakikisha chama kilichoko madarakani kinaondoshwa na kuja chama kingine mbadala, lakini kwa njia halali za kisheria-Uchaguzi huru na wa haki. Vinginevyo, haiwezekeni kudai demokrasia inajengwa Tanzania wakati vyama vinazuiwa kuishiriki!

BIASHARA

# Umemejua unavyokoleza uwekezaji vijijini, shuleni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ASHA Bakari ni mkazi wa Kijiji cha Uponda wilayani Morogoro, ambaye pamoja na wenzake 89, walikuwa wanaishi gizani kwa miongo kadhaa. Leo wanasema ni kama watu wanaoishi na jua ndani ya nyumba zao.

Ni kwa sababu wanauona mwanga kila siku na hilo limefanikishwa na Shirika la Kikristu la TCRS , lililowapa msaada wa nishati ya umeme jua. Walioupata mapema mwaka huu, ambao licha ya kuwapatia mwanga nyakati za usiku umewainua kiuchumi.

Asha mwenye miaka 61 sasa ni mwekezaji, anachaji simu muda wote na hilo ndilo ongezeko la thamani katika maisha yake na wengine baada ya kuongeza kipato na kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali.

Akizungumza mbele ya viongozi mbalimbali wa Kijiji na TCRS Asha, anasema ni mjane na msaada huo umemuokoa na kumfanya aweze kujitegemea huku akiwa na uhakika wa kipato cha kumpatia chakula na mahitaji mengine ambayo kabla alikuwa hayapati.



Asha Bakari anayefanya biashara ya kuchaji simu baada ya kupata msaada wa nishati ya umeme wa jua wa Shirika la Kikristu la TCRS. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

**MAPATO KWA SIKU**

"Kwa siku ninaweza kuletewa kati ya simu tano mpaka 10 za kuchaji, na kila simu ninachaji kwa Shilingi 300 hivyo nina uhakika wa kupata kati ya Shilingi 1,500 mpaka 3,000 kila siku kwa huduma ya kuchaji hapa kijijini." Anasema.

Anaongeza kuwa kiasi hicho cha fedha anachokipata kutokana na kuchaji simu ananunulia mahitaji ya nyumbani pamoja na ya shule ya mtoto pekee anayesoma kidato cha tatu katika Sekondari ya Tawa.

Mkuu wa Sekondari ya Tawa ambayo nayo ina umeme jua wa TCRS, Anagrace Jackson, anaishukuru taasisi hiyo, kwa msaada huo wa umeme jua na kusema shule hiyo haijafikiwa na huduma ya nishati inayotolewa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Anaeleza kuwa umemejua shuleni hapo umekuwa msaada mkubwa kwa kuwapa wanafunzi mwanga hasa wanaoishi bweni na kubadilisha maisha yao.

Pia, Mwalimu Anagrace anasema kupatikana kwa umeme huo shuleni hapo kumewasaidia katika mambo mengi ikiwamo ulinzi na usalama wa mazingira ya shule, kwa sababu awali walikuwa gizani.

> **Umemejua shuleni hapo umekuwa msaada mkubwa kwa kuwapa wanafunzi mwanga hasa wanaoishi bweni na kubadilisha maisha yao.**

"Usalama wa wanafunzi na vifaa vya shule haukuwa wa hakika. Ni kama ulikuwa hatarini."

Anaendelea kuwa umeongeza ari na mori wa wanafunzi kujisomea hasa nyakati za usiku na kuongeza wa ufaulu masomo yao na kupiga hatua kubwa kitaaluma.

Mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, Yustina Bunga, anasema umemejua umewaongezea muda wa kujisomea hususani wanafunzi wa kidato cha nne ambao kwa sasa wanajiandaa na mitihani ya mwisho.

Anasema wana uhakika wa kufanya vizuri katika mitihani hiyo kutokana na uwapo wa mishati ya kujisomea ambao unawawezesha kupata muda mrefu wa kujisomea kila wakati.

Mkazi wa Kijiji cha Milawila Kitongoji, cha Minyolopwe Rajabu Chonzo, analishukuru shirika la TCRS kwa kuyabadili maisha yake kwa msaada wa umemejua ambao alifungiwa Januari mwaka huu.

"Umenisaidia na familia yangu ya watoto watano kuokoa kiasi cha pesa ambazo tulizitumia kununua mafuta ya taa kila siku na sasa tunaziwekeza kwenye masuala mengine," anasema Chonzo.

Anasema nilitumia wastani wa Shilingi 3,000 kwa wiki kununua mafuta ya taa ambayo kwa sasa kiasi hicho cha pesa ninakitumia, kwa ajili ya kujipatia mahitaji mengine muhimu ya nyumbani." Anaongeza

**UWEKEZAJI ZAIDI SHULENI**

Anasema kati ya watoto watano alionao, wanne wanasoma ambao wawili wanasoma shule ya msingi na wawili wako sekondari, hivyo kupata nishati hiyo ya umeme jua kumewawezesha kujisomea nyakati za usiku na wamefanya vizuri kitaaluma.

"Ninawanunulia pia mahitaji ya shule, Pia imenipunguzia muda wa kwenda kutafuta kuni msituni, kwa sasa kama ni kuzitafuta basi ni kwa ajili ya kupikia tu, kwani awali tulikuwa tukiwasha moto nyakati za usiku kwa lengo la kupata mwanga, kwa kuwa kuna wakati tulikosa pesa ya mafuta ya taa." Anaeleza Chonzo na kusema kuwa fedha hizo anazitumia kununua mahitaji ya shule.

"Kama unavyoona nyumba zetu zilivyo, madirisha ni madogo mno na kuna wakati unawasha kibatari hata nyakati za mchana, ili uweze kuona vyema na moshi wa kibatari unatudhuru na kusababisha magonjwa ya kifua ,"

Muuguzi wa zahanati ya Kijiji cha Uponda, Mariam Mlelamwana, anasema umemejua umeiwezesha zahanati hiyo kutoa huduma bora hasa nyakati za usiku.

"Wapo wagonjwa ambao huja nyakati za usiku ikiwamo kina mama wanaohitaji huduma ya kujifungua ambao awali tulikuwa na umeme jua wenye uwezo wa kuwasha taa moja tu na ilikuwa inatulazimu kuwaagiza wagonjwa waje na tochi au simu usiku."

Mlelamwana, anasema vitochi hivyo mwanga wake ni hafifu na sasa hali imekuwa shwari kabisa kwani umemejua huu, una uwezo wa kuwasha taa 12 na kuiangaza hospitali.

**KUINUA KAYA MASKINI**

Awali Ofisa Mtendaji , Anderson Chitemu, analishukuru shirika la TCRS kwa msaada huo kwa kuwa umerejesha matumaini kwa kaya maskini 88 kwenye kata hiyo hapo.

Chitemu anasema licha ya msaada huo wa umeme jua huwaongezea ari na mori kwa wanafunzi wanaotoka kaya hizo kujisomea, pia una msaada mkubwa katika kuwawezesha wananchi hao kuinua kipato chao kwani wengi wao wanatumia umeme huo kuchaji simu na kupata pesa za kujikimu.

Msimamizi wa Miradi wa Shirika la TCRS Mkoa wa Morogoro, Rehema Samuel, anasema TCRS, imeona umuhimu wa kuzisaidia kaya 88 masikini nishati ya umemejua, ili kwanza kupata mwanga nyakati za usiku ambao utawawezesha kuokoa fedha ambazo wanatumia kila siku kununua mafuta ya taa.

Aidha, ni kuwasaidia katika utunzaji wa mazingira sambamba na kusaidia watoto wanaosoma kupata muda wa ziada wa kujisomea nyumbani nyakati za usiku.

Samuel anasema dhima kubwa ya shirika hilo ni kusaidiana na serikali kuleta ustawi na kubadili mtindo wa maisha ya wananchi wenye kipato cha chini kuwawezesha, ili waweze kujikwamua katika nyanja mbali mbali za maisha.

Sambamba na hilo Samuel anasema kwa kuwa moja ya shughuli za TCRS ni kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira hivyo, wanashirikiana kikamilifu katika kuwapatia wananchi hao nishati mbadala ya umemejua ili kuzuia kuharibu misitu kwa kukata kuni na mkaa.

TCRS imetoa umeme kwa kaya maskini 88 kwenye Vijiji vya Milawilila na Uponda pamoja na Shule ya Sekondari ya Kata ya Tawa na zahanati ya Kijiji cha Uponda.





## NGO 150 kushiriki maonyesho AZAKI

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ZAIDI ya mashirika 150 yasiyo ya kiserikali yanatarajiwa kushiriki katika maonyesho ya Wiki ya Azaki itakayofanyika Oktoba mwaka huu, jijini hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Haki Rasilimali, Rachel Chagonja, aliyasema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya Wiki ya Asasi zisizo za Kiserikali (AZAKI) kwa mwaka 2021.

Alisema maonyesho hayo tangu yameanza kufanyika nchini mwaka 2018, yamesaidia wananchi kupata uelewa mpana kuhusu kazi zinazofanywa na Azaki mbalimbali nchini.

"Tangu tumeanza kufanya maonyesho haya tumepata mafanikio makubwa sana ikiwamo wananchi kutambua nini Azaki zinafanya nchini lakini mwaka jana kutokana na changamoto ya ugonjwa wa UVIKO-19, hatukuyafanya lakini hali hiyo imetuwezesha kujipanga kwa ajili ya kutathmini upungufu na kujua kivingine mwaka huu," alisema Chagonja.

Alisema Wiki ya AZAKI mwaka huu itajumuisha pia maonyesho ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na mashirika hayo ikiwamo uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

"Kutakuwa na siku mbili ya kuonyesha bidhaa zinazozalishwa na asasi mbalimbali maonyesho haya yatafanyika Oktoba 23 na 24 katika viwanja vya Jamuhuri na baada ya hapo tutakuwa na midahalo ya ndani kuhusu mambo mbalimbali," alisema.

Aidha, alisema lengo la wiki hiyo pia itakuwa pia ni kujenga ushirikiano baina ya serikali, wadau, mashirika binafsi pamoja na wananchi katika kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kadhalika, alisema pia katika wiki hiyo mwaka huu pamoja na mambo mengine pia kutakuwapo na huduma za msaada wa kisheria zitakazotolewa kwa wananchi wenye uhitaji na mashirika mbalimbali.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la CBM International Tanzania, Nesia Mahenge, alisema katika wiki hiyo watahakikisha kuwa tahadhari zote za kijilinda na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19, zinachukuliwa ipasavyo.

"Niwahakikishie washiriki wote pamoja na wananchi kuwa tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona yatachukuliwa kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu wetu wa afya," alisisitiza Mahenge.

# Madini, Afya waelekeza nguvu mapambano VVU, TB migodini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Madini na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, zimejipanga katika mwaka wa fedha 2021/22 kuanza kutekeleza mkakati wa usimamizi wa masuala ya Ukimwi na Kifua Kikuu (TB) katika maeneo ya migodi.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu, Issa Nchasi, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akiwasilisha taarifa ya hali ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na TB kwenye migodi na wachimbaji wadogo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi.

Alisema mkakati huo utasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za maambukizi ya magonjwa hayo kwenye sekta ya madini.

"Tume ya Madini kupitia Idara ya Ukaguzi wa Migodi na Mazingira kwa kushirikiana na Waganga Wakuu wa Wilaya, inaendelea kufanya mafunzo kwa wachimbaji wadogo, mafunzo hayo yanalenga kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali yakiwamo maambukizi ya VVU na TB," alisema.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipongeza kamati hiyo ya Bunge kwa ushauri unaotolewa kwa sekta ya madini katika kusimamia afya za wadau wanaojishughulisha na uchimbaji madini.

Alisema mazingira ya uchimbaji mdogo kwenye maeneo yenye leseni na yenye milipuko ya madini (mineral rushes) kwa kiasi kikubwa yanakosa miundombinu wezeshi ya kulinda afya na usalama wa wachimbaji, hivyo mkakati huo utapunguza maambukizi kwa kiasi kikubwa.

"Wachimbaji wanahama kutoka eneo moja kwenda lingine kufuatana na uzalishaji wa madini. Hali hiyo inachangia ongezeko la maambukizi ya VVU na TB. Huu mkakati utapunguza maambukizi kwa kiasi kikubwa," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Alice Kaijage, alipongeza Wizara ya Madini kwa kuandaa mpango huo kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya VVU na TB katika maeneo ya migodi pamoja na wachimbaji wadogo.

"Wizara ihakikishe inatekeleza yote yaliyosemwa kwenye mkakati huu ili kutoa matokeo kwa wachimbaji," alisema.

Hata hivyo, alisisitiza elimu iendelee kutolewa kwenye maeneo yanayozunguka migodi kuhusu maambukizi ya VVU na TB.

Aliitaka Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kuhakikisha inawafikia wachimbaji wadogo kwa uhakika.

Mmoja wa maofisa kutoka TACAIDS, Nyangusi Laiser, alisema wanaendelea kutoa elimu kupitia dawati maalum katika maeneo ya migodi hapa nchini na wachimbaji wadogo ili kujikinga na maambukizi hayo.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akifungua mkutano mkuu wa kuweka mikakati ya uimarishaji wa mtandao wa barabara za mjini na vijijini, ulioandaliwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania (TARURA), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Elimu kuhusu corona kuwekewa mkazo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imejipanga kuelimisha jamii juu ya ugonjwa wa UVIKO-19 na chanjo inayotolewa kutokana na kupokea simu nyingi kutoka kwa wananchi wakitaka ufafanuzi wa masuala hayo.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana baada ya kukamilisha kikao cha kuweka mikakati ya utoaji elimu hiyo kwa kushirikiana na Idara ya Habari (MAELEZO) kilichofanyika jijini hapa.

Alisema wamekutana kuunganisha idara ya elimu ya afya kwa umma na tasnia za wizara nyingine ikiwamo Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na wanataaluma ya habari ili kuelimisha jamii juu ya ugonjwa huo.

"Wananchi wamehamasika sana kuhusu chanjo. Wanaenda kupata chanjo na mwitikio ni mkubwa na unatulazimu tuagize zingine kabla hizi zilizopo hazijaisha. Lakini kuna tatizo tumegundua ukienda kwenye simu yangu kuna meseji zaidi ya 1,000 hivyo hivyo na kwa waziri. Wananchi wamekuwa wakiuliza maswali ambayo sisi wizara tumeshatoa maelezo yake," alisema.

Alisema kutokana na maswali hayo, tayari miongozo ya wizara imeshaelekeza.

"Tumegundua watu muhimu wa kufikisha ujumbe kwa wananchi hawajashirikishwa vizuri ili kufikisha ujumbe kwa wananchi. Kwa hiyo tukasema tuwashirikishe wadau muhimu ili kufikisha ujumbe na tumeomba wenzetu wa Idara ya Habari Maelezo chini ya Gerson Msigwa (mkurugenzi) watusaidie kuratibu ujumbe unafika kwa watu wengi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya," alisema.

Naye Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema Idara ya Habari (MAELEZO) iko tayari kutekeleza maelekezo ya Naibu Waziri wa Afya na kuwataka maofisa habari nchini kuongeza kasi katika kutoa elimu na uhamasishaji wananchi kujikinga na kuchukua tahadhari zote dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

"Naibu Waziri ametaka tuongeze nguvu ya kuhamasisha wananchi kujikinga na kupokea chanjo na sisi Idara ya Habari na maofisa habari tujielekeze kuongeza nguvu zaidi kwenye elimu pamoja na vyombo vya habari niviombe tuweke msukumo zaidi na kuondoa upotoshaji na uchochezi ili Watanzania wapate chanjo na kuchukua tahadhari ya ugonjwa huu kwa kuwa upo," alisema.

Alisema wananchi wanapaswa kupata taarifa sahihi kwa wakati na si ambazo zinapotoshwa kupitia mitandao ya kijamii.



# TANROADS yaagizwa kumsimamia mkandarasi

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, ameagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), kumsimamia Mkandarasi Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group Corporation, anayejenga Barabara ya Katumba-Mbambo-Tukuyu kukamilisha mradi huo kabla ya mwezi Novemba.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kukagua mradi huo wenye urefu wa kilomita 18.7 ambao unajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 20.46 na kuagiza mkandarasi huyo kuongeza vifaa vya kufanyia kazi ili kasi ya utekelezaji iongezeke.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Busokelo kutokana na kutumika kwenye usafirishaji wa mazao mbalimbali kutoka shambani kwenda sokoni.

Alisema serikali haitamwongezea mkandarasi huyo muda wa kufanya kazi kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu bila kumaliza mradi huku akiwa na visingizio mbalimbali vikiwamo vya hali ya hewa na ucheleweshaji wa malipo.

"Nitakuja kutembelea tena barabara hii Oktoba, nataka nikute hii barabara imekamilika maana sasa hivi hana kisingizio kingine, sisi kama serikali tumeshatimiza wajibu wetu wa kumlipa fedha zake zote alizokuwa anatudai," alisema Kasekenya.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema barabara hiyo ni muhimu kwa usafirishaji wa mazao ya kilimo ikiwamo viazi mviringo na ndizi pamoja na usafirishaji wa maziwa ambayo wafugaji wanazalisha Busokelo.

Alisema Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa maeneo yenye kipindi cha mvua kirefu kuliko kiangazi na kuiomba serikali kuhakikisha mkandarasi huyo anafanya kazi kwa muda huu ambao jua linawaka ili mvua inapoanza awe amemaliza.

Alisema katika kipindi ambacho amefanya kazi katika wilaya hiyo amebaini kuwa mkandarasi wa barabara hiyo ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi isipokuwa aliyepewa tenda ya kujenga daraja la Mto Mbaka ambaye alisema anasuasua.

"Nashauri ikiwezekana mkandarasi huyu apewe na kazi ya kumalizia barabara ya kilomita moja ambazo zilikuwa zinatakiwa kufanywa na mkandarasi anayejenga daraja la Mto Mbaka, kuna mita 500 kila upande wa daraja," alisema Anney.

Pia, alisema alijaribu kuwasiliana na mkandarasi huyo mzawa anayejenga daraja hilo na kubaini kuwa hana uwezo wa kumalizia mradi huo kutokana na kuyumba kiuchumi na kwamba hata daraja hilo amechukua muda mrefu kumaliza.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa barabara hiyo, Msimamizi wa mradi huo kutoka TANROADS, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Samwel Mwambungu, alisema kwa mujibu wa mkataba, mradi huo utakamilika Novemba 14, mwaka huu.

Alisema awali serikali ilichelewa kumlipa mkandarasi huyo na kumfanya kuwa na kisingizio cha kutokulipwa na na kusimama kufanya kazi, sasa ameshalipwa fedha zote.

Vilevile, alisema kwenye eneo la mradi huo kulikuwa na miundombinu mingine ikiwamo ya maji na umeme ambayo ilikuwa inachelewesha mkandarasi kufanya kazi.

Alisema mkandarasi huyo alikuwa anasingizia mvua, kwa sasa wamembana na watahakikisha anamaliza kazi kwa muda mwafaka.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wapili kushoto), akitoa maelekezo kwa msimamizi wa mradi wa barabara ya Katumba-Mbambo-Tukuyu, wilayani Rungwe, Mhandisi Samwel Mwambungu (katikati), alipofanya ziara ya kukagua mradi huo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanafunzi wa kilimo waomba wataalamu kupima udongo

**Na Grace Mwakalinga,**MBEYA

WANAFUNZI wa Chuo cha Kilimo cha Mbalizi Polytechnic, wamewaomba wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, kupima afya ya udongo chuoni hapo ili kuendelea kuzalisha miche ya mazao kwa ubora unaotakiwa na kujiingizia kipato.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Getrude Mbembati, alisema hitaji lao kwa sasa ni kupimiwa afya ya udongo chuoni hapo kwa ajili ya kuzalisha miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda na baadaye kuiuza kwa jamii inayowazunguka.

Alisema hadi sasa TARI-Uyole wamewapatia miche na mbegu za aina mbalimbali huku wakiwapatia elimu ya namna ya kuotesha na kuhudumia mimea hiyo.

"Tunawashukuru Kituo cha Uyole kwa kutupatia elimu kilimo bora pamoja na miche ambayo tunaendelea kuitunza hapa chuoni kwetu, jambo la muhimu kwa sasa ni kuomba wataalamu kupima udongo wa hapa ili kufahamu ni aina gani ya mbegu au miche inayostahili kupandwa hapa, lakini pia tukibaini tatizo mtatusaidia kutengeneza afya ya udongo," alisema Mbembati.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema walibaini tatizo kubwa kwenye afya ya udongo na wameanzisha mradi wa kupima udongo katika mikoa minne ikiwamo Mbeya, Rukwa na Morogoro.

Alisema wataalamu wa kituo hicho watakuwa wanapima udongo ili kujua tatizo lililopo pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mkuu wa Mbalizi Polytechnic College, Essau Mwasegile, alisema wamewajengea wanafunzi uwezo wa kuzalisha mbegu za aina mbalimbali na namna ya kuhudumia.

Alisema wamewajengea uwezo wa kwenda kuwafundisha wakulima namna bora ya kilimo bora pamoja na kuwapatia ushauri wanapokabiliwa na matatizo katika uzalishaji.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, Gidion Malifimbo, alisema kwa sasa ana uwezo wa kutoa ushauri wa kilimo chenye tija kwa jamii yake na atakuwa mkulima wa mfano kwa kuzalisha kwa kuzingatia utaalamu.

# Watakaobainika udanganyifu TASAF kukiona

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, imetangaza kuwachukulia hatua za kisheria watakaobainika kufanya udanganyifu usajili wa wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF).

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua kikao kazi cha kujenga uelewa kuhusu mpango wa TASAF kipindi cha pili kwa viongozi, watendaji na wawezeshaji.

Alisema mpango wa TASAF kipindi cha pili cha awamu ya tatu umelenga kuvifikia vitongoji, mitaa na kata zote zilizosalia na hatarajii kufanyika udanganyifu.

Alisema kamati ya ulinzi imeweka ulinzi na kwamba mtumishi yeyote atakayebainika kutia doa mpango huo sheria itachukua mkondo wake huku akiwasisitiza watumishi kuwa wale wote wenye sifa zinazohitajika kwenye mpango huo waingizwe.

Serikali imekuja na mpango huu wa kipindi cha pili katika awamu ya tatu ya TASAF ili kuziba mapengo yaliyojitokeza awali na kila mwenye sifa zinazohitajika sasa atanufaika na mfuko huu, kinachohitajika ni kufanya kazi kwa weledi.

Aliwataka viongozi na watendaji wa TASAF kutopendelea badala yake watumie vigezo kuwapata wanufaika na kusisitiza familia zenye ulemavu kupewa kipaumbele.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ofisa Maendeleo, Omary Mungi alisema mpango huo utawafikia watu sahihi.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano ili kupata taarifa na watu sahihi kuingizwa kwenye mpango huo ili kuondoa malalamiko.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TASAF nchini, Cutus Mwabulanga, alisema kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kitafikia kaya 1,450,000 zenye jumla ya watu zaidi ya milioni saba nchini.

Alisema lengo la kipindi cha pili limewekwa katika kuwezesha kaya zitakazoandikishwa kwenye mpango kufanya kazi ili kuongeza kipato.

Pia, alisema watahakikisha huduma za jamii zinaongezwa na kuboreshwa ili mazingira ya upatikanaji wa elimu na afya kwa watoto yawe rafiki.

"Walengwa watakaotambuliwa na kuandikishwa katika kipindi cha pili ni kaya zinazoishi katika hali duni kwenye vijiji, mitaa na shehia zetu. Wanufaika ndani ya kaya ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaohudhuria kliniki, wanafunzi wa shule za awali, shule za msingi na shule za sekondari, mjamzito na mwanakaya mwenye ulemavu," alisema Mwabulanga.

Alisema mpango huo, unatoa ruzuku za aina mbili, ya msingi na ya masharti kwa wale ambao wanatakiwa kwenda shuleni na watoto wanaohudhuria kliniki.

Diwani wa Kata ya Isongole, Mwalingo Sothe, aliwaomba viongozi wa kata yake kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kupunguza malalamiko kwamba baadhi yao wanapendelewa.

Alisema elimu aliyoipata ya mpango huo itamsaidia kujibu maswali ya wananchi ambayo kila mara walikuwa wakiyahoji na watahakikisha walengwa wote wanaingizwa kwenye TASAF.





## TEHAMA ilivyosaidia vijana kujiajiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAENDELEO ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamesaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kutokana na wengi wao kujiajiri kupitia teknolojia hiyo. Hayo yalielezwa na Mwankina Ntile kutoka Taasisi ya Chanzo Initiative wakati wa mkutano wa kujadili mafanikio na changamoto za kutumia Mtandao Tanzania, uliofanyika kwa njia ya mtandao wa Zoom, ulioandaliwa na Shirika la Internews.

Alisema vijana wengi wamejiajiri katika huduma za kibenki na kuwa mawakala wanaotoa huduma za kifedha kupitia teknolojia ya mawasiliano ya simu za mkononi.

Alisema Tanzania kuna mawakala zaidi ya 40,000 wanaotoa huduma za kibenki na wengi wao ni vijana waliojiajiri au kuajiriwa na kupunguza ugumu wa maisha.

Alisema licha ya mafanikio hayo, kuna baadhi ya changamoto kwenye teknolojia hiyo ya habari na mawasiliano ikiwamo tozo mbalimbali zilizoanzishwa na serikali.

"Tozo zilizoanzishwa zimepunguza idadi ya watumiaji wa intaneti, lakini gharama kubwa za vifurushi vya mawasiliano," alisema. Alishauri ni vyema serikali ikaweka utaratibu wa kulinda usalama na kanuni za tozo.

Alisema bado wanawake wameachwa nyuma kwenye maendeleo ya teknolojia na mawasiliano katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kwamba ni asilimia 34 pekee ya wanawake barani Afrika wanaomiliki smartphone hususani wanaoishi mjini.

Naye Mkurugenzi wa ICT, Mulembwa Mnaku, kutoka Wizara ya ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, alisema maendeleo ya sasa ya vijana yanategemea Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kwamba kuna fursa nyingi mtandaoni, lakini bado changamoto kubwa kwa vijana ni upatikanaji wa taarifa sahihi.

Alisema ni vyema vijana wawe makini kutafuta taarifa sahihi mtandaoni ili kuepuka matatizo wanayoweza kuwapata.

Kuhusu suala la tozo za simu, Munaku alisema tayari Rais wa Tanzania Samia Suluhu ameagiza suala hilo liangaliwe upya, lifanyiwe kazi na litatolewa mwelekeo mpya na sheria zitafanywa kuwa wezeshi kwa vijana.

Kwa upande wake Shaban Maganga kutoka Internews amewataka vijana kutumia mitandao kupata fursa badala ya kufuatilia mambo yasiyo na tija.

Washiriki wa mkutano hao kutoka mikoa mbalimbali wameiomba serikali kupunguza gharama za vifurushi ili kuwawezesha watumiaji wa mitandao ya kijamii kutafuta fursa mbalimbali huku wakiomba suala la tozo za simu lifanyiwe kazi haraka.

# Mwanaharakati ataka Bodi ya Vileo ichunguzwe

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar, Ali Makame Issa, amesema Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) inapaswa kuchunguza sababu ya Bodi ya Vileo Zanzibar kutoa vibali kinyume na Sheria ya Vileo ya Namba 9 ya mwaka 2020.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, mwanaharakati huyo alisema sheria hiyo ilitungwa ili kudhibiti biashara ya vileo visiwani humo, lakini bodi imeshindwa kusimamia utekelezaji wake.

"Kwa mujibu wa kifungu 33(1) ni kampuni tatu pekee zinazoruhusiwa kuingiza vileo Zanzibar, lakini Bodi ya Vileo imeruhusu zaidi ya kampuni nane jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria," alisema Makame.

Alisema kifungu cha 28(k) kimeweka masharti baa na maduka ya pombe yawe umbali wa mita 1,000 toka sehemu ya huduma za jamii ikiwamo nyumba za ibada, shule, hospitali, madrasa na makazi, lakini Bodi ya Vileo Zanzibar imeendelea kutoa leseni bila ya kuzingatia masharti.

Alisema inashangaza sheria ya vileo imeanza kuvunjwa tangu Januari mwaka huu na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahusika kitendo ambacho ni kinyume na misingi ya utawala wa sheria hasa kwa kuzingatia watendaji wanapaswa kusimamia sheria.

Alisema kwa mujibu wa misingi ya Katiba na utawala bora viongozi wameapa kulinda sheria na haipaswi watendaji kuivunja bila ya viongozi wakuu kuchukua hatua kwa sababu ni kwenda kinyume na misingi ya utawala bora.

Mwanaharakati huyo alisema wakati serikali inalaani na kuzungumzia tatizo la kuongezeka udhalilishaji wa wanawake na watoto, lazima ikumbukwe chimbuko lake ni vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya Mzazibar ikiwamo kuongezeka kwa biashara ya vileo jambo ambalo linahitaji kushughulikiwa kwa kusimamia Sheria Namba 9 ya Mwaka 2020.

Hata hivyo, alisema ni jambo la faraja viongozi wakuu wa serikali Zanzibar wamekuwa mstari wa mbele kupambana na vitendo vya udhalilishaji vya wanawake na watoto pamoja na kusimamia misingi ya uadilifu na uwajibikaji kwa watendaji wa serikali ikiwamo kupiga vita vitendo hivyo pamoja na kuleta mabadiliko ya uwajibikaji kwa watumishi wa umma na watendaji wakuu.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Abdurazak Abdulakadir, alisema wameamua kuweka kando Sheria ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo ili kulinda maslahi mapana ya serikali katika ukusanyaji wa mapato kupitia vibali vya uingizwaji wa vileo.

Alisema serikali ya awamu ya nane imekusudia kuongeza ukusanyaji wa mapato na ndio maana waliamua kutumia busara na hekima kuweka sheria kando baada ya kupata baraka na ushauri kupitia viongozi wawili wa Ikulu Zanzibar baada ya kujitokeza utata katika utekelezaji wa sheria hiyo namba 9 ya mwaka 2020.

Akizungumzia suala la chanjo ya corona alisema wananchi wanapaswa kuungwa mkono hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Zanzibar na ya Tanzania ikiwamo wananchi kujitokeza kupiga chanjo pamoja na kuendelea kuzingatia kanuni za kujikinga na maambukizi ya corona.

Hata hivyo, alisema inasikitisha baadhi ya wanasiasa kuendeleza siasa za malumbano badala ya kusimamia siasa za kukosoana kwa nguvu za hoja na kutetea msimamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya msimamo wake wa uendeshaji wa serikali.




Makatibu wakuu kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), wakiwa katika kikao cha pamoja na makatibu wakuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT), katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Ikulu, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni maandalizi ya kikao cha kamati ya pamoja ya kushughulikia masuala ya Muungano. **PICHA: LULU MUSSA**

# Watendaji taasisi za umma watakiwa uzalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI na watendaji katika taasisi za umma wameshauriwa kuwa wazalendo na kufuata maadili ya kiutumishi wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mkurugenzi wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Khamis Kona Khamis, alisema hayo wakati akizungumza na watendaji wa Tume hiyo katika ziara ya ofisi za uchaguzi za wilaya.

Mkurugenzi Khamis alisema uzalendo ndio nyenzo muhimu kwa watumishi wa umma na utasababisha maendeleo ya haraka kwa taifa pamoja na kujenga imani kwa viongozi na watumishi.

Kona alisema katika kuimarisha ushirikishwaji na ulinzi wa maeneo ya kazi, ni vyema watendaji wa taasisi za serikali wakajenga uhusiano wa karibu na wadau wao pamoja na watu wanaowazunguka maeneo yao kwa ajili ya kurahisisha kazi zao.

Hata hivyo, Mkurugenzi Kona aliwaasa watumishi hao kudumisha usiri wa kazi zao za kila siku ili kuepukana na matatizo.

Aliahidi kuzifanyia kazi changamoto zinazozikabili ofisi za uchaguzi za wilaya ili kuendana na hadhi ya ofisi hizo kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar namba moja ya mwaka 2017.

Kwa upande wake Mkuu wa Kurugenzi ya Rasilimali Watu, Mipango na Uendeshaji Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Saadun Ahmed Khamis, aliwataka watendaji wa tume hiyo kufanyakazi kwa kushirikiana katika kuzitatua changamoto za ofisi hiyo.

Kwa upande wao maofisa wa uchaguzi wa wilaya kwa nyakati tofauti walimpongeza Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa kuamua kufanya ziara katika ofisi zao na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa katika ziara hiyo.

Kona alifanya ziara katika Ofisi za Uchaguzi za Wilaya ya Kusini, Kati na ghala dogo la Tume Kitogani kwa Mkoa wa Kusini Unguja, pamoja na Ofisi ya Uchaguzi ya Wilaya ya Magharibi 'A' kwa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Kwa Habari Motomoto**
**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MEDICAL MISSIONARY OF MARY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T287CEP** aina ya Toyota Landcruiser. Chasisi namba **JTEEB71J007017657,** Engine namba **1HZ0719884.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa: **MAN/HAN/RB/381037/2021**

116405902

## KUFUNGWA KWA KAMPUNI

Bwana **HAJI KASIMU SEFU na SANIRA MUHIDINI** wanapenda kuutangazia umma kuwa wanafunga kampuni ya **HAJI SHUKUMA LIMITED** yenye namba za usajili **Brela: 136899**

116405302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AUGUST FONGA MATEMU,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari, Yenye namba za usajili **T 683 AJC .** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . **KIL/MOS/RB/292504/2021**

116405202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika wilaya ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha MANZESE/SINZA mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi was mirathi na 181/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NDENANI XAVERY GAMA wa MAKONGO JUU KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FELIX EDWARD GAMA**

## TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe ....mwezi...mwaka...kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia.** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakama kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 7 mwaka 2021

116405102

**TAARIFA YA KAWAIDA NO.11 YA 2020**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA –ARUSHA**

**SHAURI LA MIRATHI NA 3 LA MWAKA 2021**

**ELIAIKA AMBROSE MANYANGA MWOMBAJI**
**NA**
**AMBROSE MANYANGA MAREHEMU**

**TAARIFAB YAN KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu ametajwa hapo juu wanafahamishwa kwamba ndugu **ELIAIKA AMBROSE MANYANGA** ameleta maombi yake hapa Mahakamani ateuliwe kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ambae ametajwa hapa juu.mapingamizi yeyote kuhusu maombi haya yawe yamewasilishwa hapa usimamizi wa mirathi kwa mwombaji huyu, mashauri hayo yako wazi kwa upekuzi kwa mtu yeyote.

Imewasilishwa hapa leo tarehe **28/6/2021**

HAKIMU MKAZI MKUU MFAWIDHI
ARUSHA

116406102




**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wazambia wapiga kura kumchagua rais

**LUSAKA,** Zambia

WAZAMBIA wanaamua ikiwa wanataka kumchagua tena Rais wao Edgar Lungu baada ya matokeo mabaya ya uchumi kuwahi kushuhudiwa katika miongo kadhaa na ukandamizaji dhidi ya wapinzani ambao umeibua hofu ya kuzuka machafuko.

Raia wa Zambia jana walifanya uamuzi wa kati ya Rais Edgar Lungu na mpinzani wake mkuu, Hakainde Hichilema, katika kinyang'anyiro kikali ambacho kura za maoni zilionyesha wagombea hao 'wakikabana koo'.

Mgombea Hichilema mwenye umri wa miaka 59, aliwahi kushindwa mara mbili na Lungu, mara ya kwanza katika uchaguzi wa 2015 baada ya kifo cha Rais wa zamani Michael Sata na katika uchaguzi mkuu uliofuata mwaka mmoja baadaye.

Lungu alilituma jeshi kuzima machafuko yaliyoibuka baada ya makabiliano kati ya wafuasi wa vyama vinavyohasimiana kuelekea uchaguzi wa jana wa Rais na bunge, hatua iliyokosolewa na wakosoaji kama mbinu ya kuwatisha na kuwahujumu wapigaji kura wafuasi wa upinzani.

**Hatujihisi salama kwa kuwa kuna hali isiyoridhisha nchini humo kutokana na uchaguzi unaoendelea kumpata Rais na wabunge.**

Msemaji wa chama cha Rais Lungu cha (Patriotic Front), PF, Antonio Mwanza, alidai siku ya Jumanne kwamba upinzani unatumia machafuko kuvuruga na kufuja mchakato wa uchaguzi na kuwatisha watu ili wasijitokeze kwa wingi kutumbukiza kura zao kwenye masanduku vituoni.

Wachambuzi walisema matokeo ya uchaguzi huo unaoshuhudia wagombea wakipambana kwa karibu na kukaribiana, yatatoa muelekeo kwa uwekezaji katika nchi hiyo yenye utajiri wa shaba, ambako zaidi ya nusu ya wakazi wake milioni 17 wanaishi katika hali ngumu ya umasikini.

Utafiti ulibainisha kuwa hali ngumu ya kiuchumi imepunguza umaarufu na uungwaji mkono wa Lungu, anayetuhumiwa kwa kuchukua mikopo mikubwa bila mpango kufadhili miradi ya kifahari ya ujenzi wa miundombinu, huku kwa upande mwingine gharama za maisha zikipanda.

Wapigaji kura wa upinzani, ambao rangi ya chama chao ni nyekundu, wametulia bila kuonyesha hamasa kubwa katika mji huo ambao ni ngome ya chama tawala, pia baadhi yao wanavaa nguo za rangi ya kijani ili kuepuka kutumbukia kwenye matatizo, katika kile kinachofahamika kama 'mbinu ya matikiti maji'.

William Njombo, mfuasi wa chama cha upinzani cha (UPND), alisema kwamba hawajihisi salama kwa kuwa kuna hali isiyoridhisha nchini humo kutokana na uchaguzi unaoendelea kumpata Rais na wabunge.

Ubalozi wa Marekani mjini Lusaka ulihimiza polisi ya Zambia na jeshi kutumia sheria kwa usawa na kwa kuheshimu ubinadamu wakati wa uchaguzi wa jana. Huku machafuko yakiwa ni ya kawaida katika uchaguzi wa Zambia, kila mabadilishano ya madaraka yamefanyika kwa njia ya amani tangu nchi hiyo ambayo ni koloni la zamani la Uingereza ilipoanzisha siasa za vyama vingi mnamo 1990.

Hichilema na Lungu walifanya kampeni wakijinasibu kama 'wanasiasa wa watu' wakiahidi ajira na utajiri kwa wapiga kura, zaidi ya watu milioni saba waliandikishwa rasmi kupiga kura katika uchaguzi wao huku matokeo yakitarajiwa kutangazwa siku ya Jumapili.

Ofisa Mkuu wa tume ya uchaguzi, Patrick Nashindano, aliahidi uchaguzi utakuwa huru na wa haki. Pia alisema tume hiyo haijishughulishi na mizengwe na uchakachuaji wa matokeo.

Matokeo ya Lusaka, mji wenye wakazi zaidi ya milioni 3.3 na mkoa wa kati wenye utajiri wa madini ya shaba, yatakuwa na umuhimu mkubwa katika kuamua mshindi. Sydney Chilong, mfanyabiashara anayeuza nguo mjini humo anasema ana matumaini watafanikiwa kuilinda amani lakini anadhani kitakuwa kipindi kigumu chenye changamoto kwao.**DW**



Mwananchi nchini Zambia akishiriki kupiga kura katika uchaguzi uliofanyika jana wa kumchagua rais na wabunge. **PICHA AFP**

## Mafuriko yaua 52 Niger

**NIAMEY,** Niger

SERIKALI nchini Niger imesema kuwa takribani watu 52 wamepoteza maisha katika mafuriko yaliyotokea nchini humo, huku wengine 34 wakijeruhiwa na maelfu wakipoteza makazi yao na kukosa pa kujihifadhi.

Kwa mujibu wa ripoti ya ufuatiliaji ya ulizi wa raia, idadi hiyo ya waliopoteza maisha ni pamoja na watano waliokufa kati ya Jumanne na Jumatano baada ya mvua kubwa iliyonyesha mji mkuu wa Niamey na kusababisha uharibifu mkubwa ikiwemo kuharibu makazi.

"Zaidi ya nyumba 4,000 na vibanda 200 vilianguka na mifugo 800 ilisombwa na maji, Mikoa kadhaa ya nchi imeathiriwa na mafuriko ambayo yamekuwa yakitokea tangu mwanzo wa Juni.

"Mji mkuu ni miongoni mwa miji iliyoathiriwa zaidi na mvua ya milimita 144 ilirekodiwa kati ya Jumanne na Jumatano, watu wasiopungua 70 walipoteza maisha kutokana na mafuriko nchini Niger mwaka jana na wengine 350,000 waliathirika," ilisema. **BBC**



## Uteuzi wa Tambwe wazua sintofahamu

**KINSHASA,** DRC

UTEUZI wa aliyekuwa kiongozi wa waasi, Emmanuel Tommy Tambwe, kuwa mratibu wa mpango wa serikali wa kupokonya silaha mikononi mwa raia na makundi ya waasi Mashariki mwa DRC, umeendelea kukosolewa.

Julai 4, 2021 rais Felix Tshisekedi alisaini agizo ambalo liliunda mpango wa P-DDRCS.

Mpango huu mpya uko chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya rais wa jamhuri. Moja ya malengo ni kupata ufadhili wa kimataifa na kuwapa wapiganaji wa zamani fursa ya kujumuika tena katika jamii zao.

Zaidi ya mwezi mmoja baada ya kuanzishwa kwa programu hiyo, maofisa wakuu wa mpango huo waliteuliwa. Mara tu baada ya majina hayo kutangazwa, kulizuka utata kuhusu uteuzi wa Emmanuel Tommy Tambwe Ushindi, ambaye ni mratibu wa mpango huo.

Mnamo 2002, wakati akiwa naibu wa gavana wa mkoa wa Kivu Kusini kutoka kundi la waasi la RCD, alitajwa na shirika la Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (RSF) na shirika la kimataifa la Haki za Binadamu la Amnesty International kama mdhamini wa visa vya kukamatwa kwa waandishi wa habari, ambao wengi wao walikamatwa na kudhalilishwa.

Akiwa bado anafanya kazi na makundi ya waasi, mwaka 2012, aliliongoza kundi moja lenye uhusiano wa karibu na waasi wa M23, lililojulikana kama Muungano wa Ukombozi wa Mashariki mwa Congo.

Ripoti ya kundi la wataalamu wa Umoja wa Mataifa lilieleza kuwa Tambwe alikuwa akitetea hasa kuundwa kwa jimbo huru la Kivu.

"Mbaya zaidi kundi alilokuwa akiongoza Emmanuel Tommy Tambwe Ushindi linadaiwa kuwa lilifanya uhalifu huko Kivu Kusini, pamoja na kuajiri watoto kwa nguvu," ilisema. **RFI**

HABARI MICHEZO

# MESSI: NDOTO YANGU KUSHINDA UEFA NA PSG




**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi amesema ndoto yake ni kushinda kwa mara nyingine tena kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kujiunga na Paris St-Germain, akiongeza: "Nafikiri tuna timu ya kufanya hivyo hapa."

Nahodha huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 34, alishinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona, kwa mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2015.

PSG bado inatafuta taji lake la kwanza la mashindano hayo, na ilifungwa kwenye fainali na Bayern Munich mwaka jana.

"Malengo na ndoto yangu ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara nyingine zaidi," amesema Messi baada ya kutambulishwa kuwa mchezaji wa PSG.

Messi aliondoka Barcelona - ambaye alijiunga nayo tangu akiwa na umri wa miaka 13, walishindwa kumpatia mkataba mpya kutokana na sheria na kanuni za kifedha za LaLiga kutoruhusu.

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote duniani, akifunga mabao 672 kwenye mechi 778 kwa miamba hao wa Katalunya.

Alishinda tuzo ya Ballon d'Or mara zita na alibeba jumla ya mataji 35 kwa kipindi chote alichokaa pale Nou Camp, lakini alisema amepata hamasa kubwa "wakati huu kuanza maisha mapya" baada ya "ugumu" wa kuondoka Barcelona.

# United, Arsenal zamgombea Tolisso



**LONDON,** England

KWA mujibu wa ripoti za magazeti ya Ulaya, klabu za Ligi Kuu England, Manchester United na Arsenal zinagombea huduma ya kiungo wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Corentin Tolisso.

Mfaransa huyo ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha Kocha Didier Deschamps katika michuano ya Euro 2020 msimu huu, anatarajiwa kuondoka kwa miamba hiyo ya Ujerumani baada ya kusajiliwa kwa mbwembwe nyingi mwaka 2017, kwa dau la pauni milioni 38 akitokea Lyon.

Gazeti la Bild la Ujerumani limesema, Tolisso mwenye umri wa miaka 26 amebakiza mkataba wa mwaka mmoja na Bayern inakusudia kuachana na mchezaji huyo kwa ada iliyopunguzwa hadi pauni milioni 8.5.

Kocha mpya wa Bayern, Julien Nagelsmann ana nia ya kumsajili kiungo Marcel Sabitzer kutoka klabu yake ya zamani ya RB Leipzig na atalazimika kuuza mchezaji, ili kufanikisha dili hilo, huku Tolisso akiwa mtarajiwa mkuu wa kuondoka.

# Shaqiri akubaliana na Lyon

**LYON,** Ufaransa

NYOTA wa Liverpool, Xherdan Shaqiri amefikia makubaliano binafsi wakati kukiwa na uwezekano mkubwa wa kuhamia Lyon, lakini klabu hizo mbili bado haijafikia makubaliano ya ada yake.

Shaqiri alikuwa sehemu ya kikosi cha Liverpool msimu uliopita, akicheza mechi 14 za Ligi Kuu England ingawa hakufunga bao lolote.

Alitumika zaidi msimu wa 2019/20, akitoa mchango wake wakati wekundu hao wakitwaa taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.


Shaqiri yupo kwenye mwaka wake wa mwisho na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo hivi karibuni, huku Lyon na Lazio zimekuwa zikihusishwa na uwezekano wa kumsajili.

Na kwa mujibu wa L'Equipe timu yake ya zamani ya Lyon ndio inayoonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kushinda kwenye mbio za kuwania saini hiyo.

Miamba hao wa Ligue 1 wameripotiwa, kwamba wameshafikia makubaliano binafsi na Shaqiri.

Na mshahara wake unatajwa kwamba, atalipwa euro 90,000 kwa wiki na amepewa ofa ya mkataba wa miaka mitatu pale Lyon, wakati klabu hiyo ikitafuta mbadala wa Memphis Depay.

Depay alijiunga na Barcelona baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu uliopita na alikataa kusaini mpya.



# Tuchel atoa siri ya Kepa Chelsea iking'ara

**BELFAST,** Ireland Kaskazini

THOMAS Tuchel ameelezea sababu ya kufanya mabadiliko ya golikipa kipindi cha dakika za mwisho za muda wa ziada, kuwa ilikuwa ni sehemu ya mbinu za mchezo, huku Kepa Arrizabalaga akiokoa penalti mbili na kuisaidia Chelsea kushinda taji la Uefa Super.

Bao la Gerard Moreno la kipindi cha pili lilisawazisha lile la uongozi la Hakim Ziyech pale kwenye dimba la Windsor Park, na kusababisha mchezo kwenda kwenye changamoto ya penalti, wakati Tuchel akimwingiza Kepa kuchukua nafasi ya Edouard Mendy dakika za mwisho.

Golikipa huyo raia wa Hispania, aliokoa penalti mbili za Aissa Mandi na Raul Albiol kwenye mikwaju hiyo na kuifanya Chelsea kushinda 6-5 na kulitwaa taji la Uefa Super Cup kwa mara ya pili katika historia yao.

Akizungumza na BT Sport baada ya mchezo huo, Tuchel alielezea uamuzi wa kumwingiza Kepa yalishajadiliwa awali pamoja na ushauri wa kocha wa magolikipa.


"Haikuwa sababu ya kutokuwa na imani," alisema Tuchel akijibu swali aliloulizwa kuhusu mabadiliko dakika za mwisho za muda wa ziada.

"Tulizungumza na magolikipa baada ya mchezo wa kwanza dhidi ya Barnsley. Tuliangalia takwimu. Tulikuwa tumejiandaa mapema."

"Kepa ana asilimia kubwa ya kuokoa penalti. Tulizungumza na wachezaji kwamba hilo litatokea kama timu itakuwa na mechi za mtoano.

"Kwa uzuri ni kwamba Edouard (Mendy) mwenyewe alilipokea hili vizuri sana.

"Kuna uthibitisho Kepa ni bora zaidi kwenye nidhamu. Wote ni wachezaji wa timu. Edouard hakuonyesha kuchukia wakati akiondoka uwanjani. Alikuwa na furaha kwa sababu ya kuisaidia timu."





# GREALISH KUWATOA JESUS, SILVA

**MANCHESTER,** England

BAADA ya kukamilisha usajili wa Jack Grealish, Manchester City imeripotiwa kuwaweka sokoni wachezaji wake wawili, ili kuendana na masuala ya kiuchumi.

Grealish amejiunga na City kwa mkataba wa miaka mitano akitokea Aston Villa mapema wiki iliyopita.

Huo ni usajili ambao umeweka rekodi kwenye historia ya soka la Uingereza kwa ada iliyotolewa, ambayo ni pauni milioni 100.

Usajili huo ulivunja rekodi ya pauni milioni 93.5 zilizotolewa na Manchester United wakati walipomrudisha Paul Pogba pale Old Trafford mwaka 2016.

Na kwa mujibu wa ripoti, majina ya wachezaji walioripotiwa kuwekwa sokoni na City ni Gabriel Jesus na Bernardo Silva.

Wachezaji hawa wamekuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi cha kocha Pep Guardiola hasa msimu uliopita, lakini sasa ni dhahiri, watapata wakati mgumu baada ya ujio wa Grealish pengine na Harry Kane ambaye pia anahusishwa na klabu hiyo.

# Nemanja ataka taji la EPL

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Nemanja Matic amesema anatamani kushinda taji la Ligi Kuu England akiwa na kikosi hicho msimu huu.

Matic ni mmoja wa wachezaji wenye uzoefu mkubwa kwenye kikosi cha United ambaye anataka kuona taji la EPL linatua hapo Old Trafford.

Matic alijiunga na United akitokea Chelsea na alifanikiwa kutwaa taji la EPL akiwa na The Blues.

Mkongwe huyo kwenye kikosi cha kocha Ole Guner Solskjaer hajafanikiwa kutwaa kombe hilo na kikosi hicho na sasa anatamani sana kufanikisha hilo akiwa ndani ya jezi nyekundu ya mashetani wekundu hao.

Akizungumza na televisheni ya United, Matic amenukuliwa akisema: "Kwa uhakika kabisa nataka kubeba taji la Ligi Kuu nikiwa hapa.

"Kwangu kombe la EPL ndio kombe muhimu zaidi. Ni kweli, Ligi ya Mabingwa Ulaya ni mashindano mazuri kushiriki, unapambana na timu kubwa za Ulaya. "Lakini, kwangu binafsi, EPL ndio kitu ninachotaka kushinda na Manchester United. Kama siku moja hili litatokea, nitakua na furaha sana."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# USAJILI WAMWEKA KLOPP NJIA PANDA

Atakiwa kuuza kwanza wachezaji waliopo ili apate nafasi ya kunasa nyota mpya ambaye...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amedokeza kwamba, Liverpool haitafanya usajili wowote kipindi hiki cha majira ya joto, mpaka pale wachezaji wengine watakapoondoka klabuni hapo.

**Ibrahima Konate umekuwa usajili pekee uliowasili hapo kwenye dimba la Anfield kipindi hiki cha majira ya joto, akijiunga kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 36 akitokea RB Leipzig, Juni mwaka huu.**

Wameuzwa wachezaji wachache, huku Harry Wilson akijiunga na Fulham, Taiwo Awoniyi akihamia Union Berlin na Marko Grujic akienda kwa mkopo kule Porto.

Nyota Georginio Wijnaldum amejiunga na Paris Saint-Germain kwa uhamisho huru baada ya Liverpool kushindwa kumshawishi kuongeza mkataba mpya kiungo huyo.

Wekundu hao wamekuwa wakihusishwa na wachezaji kadhaa wa kuziba pengo la Wijnaldum, wakitajwa Saul Niguez na Renato Sanches, lakini hakuna dili lililofanyika hadi sasa.

Na usajili sasa unaonekana kuwa mgumu kama hawatauza wachezaji kwa mujibu wa Klopp wakati akielezea kwenye mahojiano na TV2.

"Kipindi hiki cha majira ya joto dirisha la uhamisho lipo wazi, hivyo wengi wanatarajia kuona usajili wa wachezaji wapya, tunaona nini kitatokea," alisema raia huyo wa Ujerumani.

"Hebu tuangalie kikosi. Unataka kununua mlinzi wa pembeni? Golikipa mpya? Tayari tuna wachezaji pale.

"Kwenye safu ya kiungo tuna wachezaji wengi kama Thiago, Fabinho, Henderson, Alex Oxlade-Chamberlain na Naby Keita. Kwa nyongeza tuna wachezaji wanaovutia ambao ni vijana kama Harvey Elliott na Curtis Jones.

"Kwenye ushambuliaji tuna Sadio Mané, Roberto Firmino, Mohamed Salah, Diogo Jota, Xherdan Shaqiri, Takumi Minamino na Divock Origi.

"Hivyo hakuna namna yoyote ya kufanya usajili bila kuuza kwanza wachezaji wengine."

## ZISIKUPITE

### MESSI AIDAI BARCA

BARCELONA bado wanadaiwa na mshambuliaji wao wa zamani wa Argentina, Lionel Messi, 34, euro milioni 39 kama sehemu ya bonasi ya uaminifu iliyojumuishwa katika mkataba wa mwisho wa mchezaji huyo wa Paris St-Germain. ***(El Espanol, via 90min)***

### LUKAKU HUYOOO CHELSEA

ROMELU Lukaku, 28, anakaribia kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 97.5 kutoka Inter Milan kwenda Chelsea, baada ya mshambuliaji huyo wa Ubelgiji kusafiri kwenda London Jumatano jioni. ***(Sky Sports)***

### RAMSDALE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL ipo kwenye mazungumzo ya hali ya juu na Sheffield United kwa ajili ya kumsajili golikipa wa England, Aaron Ramsdale (23), na washikabunduki hao wakilazimika kulipa ada ya mwanzo ya pauni milioni 24 ambayo inaweza kuongezeka hadi pauni milioni 30 na nyongeza. ***(Football. London)***

### VARANE, UNITED SAFI

MANCHESTER United itatangaza kumsajili beki wa kati wa Ufaransa, Raphael Varane kutoka Real Madrid ndani ya saa 24 zijazo, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kumaliza vipimo vya matibabu Jumatano.***(Sun)***

### ABRAHAM KIMEELEWEKA

CHELSEA wamekubali dau la pauni milioni 34 kutoka AS Roma kwa ajili ya mshambuliaji wake, Tammy Abraham, 23. ***(Goal)***

### LACAZETTE ATOLEWA

ARSENAL itamtoa mshambuliaji wake wa Ufaransa, Alexandre Lacazette, 30, ili kumrahisishia njia Tammy Abraham kuhamia kwa washikabunduki hao. ***(Calciomercato)***

### SEVILLA NA KOUNDE

SEVILLA wako tayari kumuuuza mchezaji anayelengwa na Chelsea, Jules Kounde, 22, lakini Blues hao hawataki kuafiki kifungu cha kumchukua mlinzi huyo wa Ufaransa. ***(Evening Standard)***

### VESTERGAARD SOKONI

KLABU ya Southampton imekubali dau la pauni milioni 15 kutoka kwa Leicester City ili kumwachia mlinzi wake raia wa Denmark, Jannik Vestergaard, 29. ***(Daily Echo)***

### SPURS, VILLA ZATETA

TOTTENHAM Hotspur na Aston Villa wote wanaandaa ofa kwa kiungo wa Southampton na raia wa England, James Ward-Prowse, 26. ***(Telegraph)***

### SHAQIRI NJIA MOJA

LYON wanafanya mazungumzo na Liverpool juu ya makubaliano ya kumsajili kiungo wa wekundu hao mwenye umri wa miaka 29, Xherdan Shaqiri. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

# AZAM KUELEKEA ZAMBIA KUIMARISHA NYOTA WAKE

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kuondoka nchini na kuelekea katika mji wa Ndola nchini Zambia kwa ajili ya kuweka kambi ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki, imefahamika.

**Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema kikosi hicho kikiwa Zambia kitacheza mechi mbalimbali za kirafiki na tayari mazungumzo na klabu za huko yameshaanza.**

Kikosi cha kwanza cha Azam FC kiliingia kambini mapema wiki hii kikiwa chini ya Kocha Mkuu, George Lwandamina.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alikataa kuliambia gazeti hili mahali ambapo timu yao inakwenda kujifua.

Popat alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata mechi nyingi za kirafiki za kimataifa na kitaifa kwa ajili ya maandalizi kuelekea michuano ya CAF ambayo inatarajia kuanza mapema Septemba, mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema wamejipanga kukiimarisha kikosi chao kwa kucheza michezo na timu zenye uzoefu ili kuwaweka tayari wachezaji wao kukabiliana na ushindani wanaoutarajia kwenye msimu ujao.

"Tayari tumeshaingia kambini na kuanza mazoezi, na ndani ya wiki hii kikosi kinatarajia kwenda nje ya nchini kwa ajili ya 'Pre Season', itakayokuwa na mechi za kirafiki za ushindani ili kujiandaa na michuano ya kimataifa," alisema Popat.

Kiongozi huyo alisema anaamini mahali ambapo watapachagua patawasaidia kiufundi kufikia malengo baada ya kurekebisha changamoto walizokutana nazo katika msimu uliomalizika.

"Muda utakapowadia tutaweka wazi ni nchi ipi ambayo tutaenda kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, huko tutakapokwenda tunaamini kutatusaidia katika kufikia malengo yetu," Popat alisema.

Licha ya mtendaji huyo kutoweka wazi nchi, gazeti hili lilipata taarifa kwamba kikosi cha timu hiyo kitaenda nchini Zambia na tayari maandalizi ya kambi hiyo ilifanywa mapema sana.

Chanzo chetu kiliongeza Azam ilimtuma kiongozi huyo (Popat), kwenda Zambia kuweka mazingira mazuri ya mahali ambapo kikosi kitaishi na kufanya mazoezi kwa muda wote watakaokuwa humo.

Azam FC iliyomaliza msimu uliopita katika nafasi ya tatu nyuma ya mabingwa, Simba na Yanga iliyoshika nafasi ya pili, itashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika sambamba na Biashara United iliyomaliza ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.




Mtaalamu wa Huduma za Ziada wa Tigo, Nurdin Lugembe (kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa shindano la Tigo Kandanda uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo washindi mbalimbali watajinyakulia zawadi za zaidi ya Sh. milioni 18. Kulia ni Balozi wa Kampeni ya Tigo Kandanda, Shaffih Dauda. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Tigo Kandanda yazinduliwa D'Salaam*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha jamii inaendelea kupata burudani nchini, kampuni inayoongoza kwa maisha ya dijitali Tanzania, Tigo, jana ilizindua rasmi shindano la Tigo Kandanda.

Washindi wa shindano hili, watakuwa wakipatiwa kwa kujibu maswali mbalimbali ya mchezo wa soka kupitia ujumbe mfupi wa maneno na watajishindia zaidi ya Sh. milioni 18.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mtaalamu wa Huduma za Ziada wa Tigo, Nurdin Lugembe, alisema, "Kwa miaka mingi tumekuwa tukitafuta njia ambazo wateja wetu wanaweza kushirikiana na Tigo kwa faida ya kuingiza kipato.

"Tigo Kandanda inaingia sokoni kama huduma mpya ya ubunifu ambayo itawapa wateja wa Tigo muda wa ziada kutumia simu zao kwa lengo la kujipatia pesa, mwaliko utatumwa kupitia sms kwa mteja wa Tigo, ambaye ataweza kuanza kucheza kwa kujibu maswali moja kwa moja yanayohusu mchezo wa soka," alisema Lugembe.

Aliongeza washindi watakuwa wakijishindia zawadi kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. milioni 18, simu za mkononi na vocha za kufanya manunuzi katika duka la nguo la Shafii Dauda.

Naye Balozi wa kampeni ya Tigo Kandanda, Shaffih Dauda, alisema amefurahi kuchaguliwa kuwa balozi wa kampeni hiyo na anaamini wateja watakaojishindia zawadi watafurahia shindano hilo.

## Biashara United mguu sawa CAF

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya, uongozi wa Biashara United wamewasajili nyota wawili wapya, Aniset Revocatus kutoka Mwadui FC na Notikely Masasi wa Ken Gold, ambaye aliwahi pia kuichezea Mbeya City.

Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema wanaendelea vyema na mchakato wa usajili licha ya muda uliobakia wa kufungwa kwa dirisha la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ni keshokutwa.

Alisema pia wanatarajia kucheza mechi mbalimbali za kirafiki kwa lengo la kuwaweka tayari wachezaji wao, lakini kuendelea kuboresha idara zenye changamoto.

"Ni kweli tumekuwa na kasi kwenye usajili kwa sababu tunakimbizana na muda, mwisho ni Agosti 15, mwaka huu na inatakiwa tuwe tumekamilisha," alisema Mataso.

Mbali na wachezaji hao, Biashara United imeshatangaza kuwasajili nyota mbalimbali akiwamo nyota wa zamani wa Yanga, Atupele Green, Kassim Mdoe kutoka Tanzania Prisons na Tayo Odongo wa Zoo ya Kenya.

## KMKM, Express FC zapigwa faini

**Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamepigwa faini ya zaidi ya Sh. milioni 10 kwa kosa la utovu wa nidhamu wakati wenzao Express FC kutoka Uganda wakitakiwa kulipa Sh. milioni nane kwa makosa ya utovu wa nidhamu.

Kamati ya Nidhamu ya mashindano ya Kombe la Kagame ilizikuta na makosa klabu hizo, kabla hazijakutana katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza iliyochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambapo Express ilisonga mbele kwa penalti.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa CECAFA, Rogers Mulindwa, alisema faini hizo zimetokana na makosa ya utovu wa nidhamu waliyofanya pamoja na kugoma kufanya mazoezi ya kupasha misuli katika vyumba vya kubadilishia nguo na kuchelewesha muda wa kuanza mechi.

Alisema naye Kocha Mkuu wa Express FC, Wasswa Bbosa, ameonywa vikali kwa kosa lake la kutoa maneno machafu kwa waamuzi wa mchezo huo walioongozwa na Malong Ring kutoka Sudan Kusini.

# Michezo

Ijumaa Agosti 13, 2021
Nipashe



Usajili wamweka Klopp njia panda UKURASA 22



Kocha wa viungo wa Simba, Adel Zrane (kulia), akiongoza mazoezi ya timu hiyo iliyoweka kambi jijini Rabat, Morocco kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# YANGA YACHEZA KARATA 2021/22

## Yamtema Ukonde mapema huku ikimwashia taa...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya Kombe la Kagame yanayoendelea hapa nchini, uongozi wa Yanga umetangaza kuachana na mchezaji, Jimmy Ukonde raia wa Msumbuji ambaye alitarajiwa kuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2021/22.

**Hata hivyo Yanga imemtangaza rasmi kiungo, Dickson Ambundo aliyekuwa akichezea Dodoma Jiji FC kuwa ni mchezaji wake mpya, lakini wakiendelea na mchakato wa usajili.**

Tayari Yanga imeshawatambulishwa nyota wake wengine wa kigeni wote raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambao ni pamoja na Heritier Makambo na Fiston Mayele.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili wanatarajia wakati wowote kuwatangaza wachezaji wengine wapya, wawili wa kigeni na mmoja Mtanzania ili kuhitimisha usajili wa msimu wa 2020/21 na baadaye kujiandaa na safari ya kuelekea Morocco kuweka kambi.

"Tumesajili wachezaji 12, nane wa kigeni na wanne wa ndani. Bado wawili wa kimataifa ambao hatujawatangaza na mmoja wa ndani. Nadhani ndani ya siku chache kuanzia kesho (leo), tunaweza kuwatangaza na hapo tutakuwa tumemaliza usajili, safari ya kwenda Morocco itakuwa imeiva," alisema Bumbuli.

Alipoulizwa kama mmoja wa wachezaji hao ni Ukonde ambaye alionekana kutumikia timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Kagame, Bumbuli alisema kwenye orodha ya wachezaji wawili ambao hawajatangazwa hakuna jina lake.

"Kwa wachezaji wa kimataifa sidhani kuna nafasi ya kwenda naye (Ukonde) Morocco. Kwa orodha niliyonayo sidhani kama yupo. Hakukuwa na nafasi ya kumpa mkataba. Tusubiri, lakini kwa hali ya kawaida sidhani kama kuna nafasi yake. Kifupi tu mimi nina majina mawili ya wachezaji wa kigeni, yeye hayumo," Bumbuli alisema.

Yanga iliwafanyia majaribio baadhi ya wachezaji kwenye michuano ya Kombe la Kagame, Ambundo na baadhi ya wachezaji wachache wa kikosi cha U20 wakionyesha kiwango kizuri, lakini kwa upande wa Ukonde, baadhi ya wanachama na mashabiki wa klabu hiyo hawakuridhishwa na kiwango chake.

Yanga ilimuona Ukonde akiwa na klabu ya UD Songo ya Msumbiji ambayo pia alikuwa akiichezea Luis Miquissone anayekaribia kujiunga na vigogo wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Katika kuendelea kujiimarisha, Yanga iliamua kutangaza kuachana na aliyekuwa golikipa wake chaguo la kwanza, Metacha Mnata na msaidizi wake Mkenya Farouk Shikalo na nafasi zao kuchukuliwa na Djigui Diara raia wa Mali na Mtanzania Erick Johora aliyekuwa akiichezea Aigle Noir ya Burundi.

Yanga imeshindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu minne mfululizo huku pia ikishindwa kufanya vyema kwenye mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake hushiriki michuano ya kimataifa.

## Simba kuanza na vigogo CAF

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI winga mpya wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba, Peter Banda jana alikabidhiwa rasmi jezi namba 11, ambayo ilikuwa inavaliwa na kiungo mshambuliaji, Luis Miquissone, Wekundu wa Msimbazi wataanzia raundi ya pili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba inaanzia raundi ya pili katika michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya msimu uliomalizika kufika hatua ya robo fainali.

CAF inatarajia kuendesha droo ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na michuano ya Kombe la Shirikisho leo huko jijini Cairo.

Mbali na Simba, Yanga pia leo itafahamu mpinzani wake katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika sambamba na Azam FC na Biashara United ya Mara zitakazochuana katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Banda amejiunga na Simba wiki iliyopita na amemaliza tetesi za hatima ya Miquissone ambaye dili lake la kujiunga na Al Ahly lilikuwa halijawekwa hadharani na klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Nyota huyo jana alionekana akiwa amevaa jezi hiyo wakati wakielekea kwenye mazoezi ya timu yao iliyoweka kambi nchini Morocco, kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yatakayoanza mapema mwezi ujao.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ezekiel Kamwaga, amesema anashangaa kuona baadhi ya waandishi na wachambuzi wa habari wanaulizia dili la Miquissone limefikia hatua zipi, wakati klabu hiyo haijawahi kutamka popote pale kuwa imepata ofa ya kumuuza mchezaji huyo.

Kamwaga pia amewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kujiandaa na tamasha la Wiki ya Simba, maarufu kama Simba Day ambalo litafanyika Agosti 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >